



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS**

**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI – OFISI YA RAIS,
MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA,
MHE. KAPT. (MST.) GEORGE H. MKUCHIKA (MB.) KUHUSU
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA
MWAKA 2020/21**

APRILI, 2020

**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI – OFISI YA RAIS,
MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA
BORA, MHESHIMIWA *KAPT. (MST.)* GEORGE H.
MKUCHIKA (MB) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO
NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2020/21**

UTANGULIZI

1. *Mheshimiwa Spika*, naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa iliyochambua bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu (Fungu 20 na 30); Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma (Fungu 33); Menejimenti ya Utumishi wa Umma (Fungu 32); Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma (Fungu 67); Tume ya Utumishi wa Umma (Fungu 94); Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma (Fungu 09); na Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa (Fungu 04); Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/20. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Mpango wa Utekelezaji na Makadirio ya Fedha kwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2020/21.

2. *Mheshimiwa Spika*, Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kutujalia amani na utulivu ambavyo vimetuwezesha kutekeleza majukumu ya kuongoza Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na kuwashudumia wananchi. Aidha napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa imani kubwa aliyonayo kwangu na kunateua nimsaidie

kufanya kazi katika Ofisi yake. Ahadi yangu kwake ni kutekeleza kazi zangu kwa juhudini, uadilifu, utii na uaminifu ili kukidhi matarajio ya Wananchi. Vile vile, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dkt. Mary M. Mwanjelwa (Mb.) kwa kunisaidia katika kazi za kila siku za kuiongoza Ofisi yangu. Kwa namna ya pekee namshukuru Mungu kuwa tumepata nafasi nyingine ya kukutana tena kupokea utekelezaji wa Ofisi yangu na kutafakari malengo yajayo katika mkuutano huu wa 19 na wa mwisho wa Bunge la 11.

3. *Mheshimiwa Spika*, kwa namna ya pekee naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Jimbo la Bukoba Vijijini na Makamu wake Mheshimiwa Mwanne Ismail Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum Tabora kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri mzuri walioutoa wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2019/20 na Mapendekezo ya Mpango wa Utekelezaji na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa Mwaka wa Fedha 2020/21. Maoni, ushauri na ushirikiano wa Kamati umetuwezesha kuboresha maandalizi na utendaji kazi wa Ofisi yangu.

4. *Mheshimiwa Spika*, naomba pia, kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuiongoza nchi yetu kwa ufanisi na mafanikio makubwa tangu alipochaguliwa Mwaka 2015. Sote tumeshuhudia utekelezaji wa malengo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2015 na ahadi alizozitoa kwa wananchi wakati wa uchaguzi. Uongozi wake mahiri umedhihirika kwa jinsi anavyopambana na rushwa, ufisadi na ubadhirifu wa rasilimali za Umma. Aidha, Mheshimiwa Rais nyakati zote amekuwa akihimiza uadilifu, uwajibikaji, uchapakazi na utendaji wenye matokeo katika Utumishi wa Umma hali ambayo sote ni mashahidi kuwa Utumishi wa Umma umeimarika. Vile vile, usimamiaji mahiri wa miradi mikuu ya kimkakati kwa Taifa ni jambo ambalo kila mmoja wetu ameliona na hatuna budi kujivunia. Pili, nampongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa namna anavyomsaidia Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

5. *Mheshimiwa Spika*, Pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa uongozi wake shupavu na nia yake thabiti ya kuleta maendeleo Zanzibar na kuimarisha muungano, amani na utulivu. Vile vile, nampongeza

Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuendelea kuwatumikia wananchi wa Zanzibar kwa moyo wake wote.

6. ***Mheshimiwa Spika***, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuwa nguzo muhimu ya usimamizi na uratibu wa kazi za kila siku za Serikali Bungeni. Kwa kipindi chote cha Bunge la 11 amedhihirisha umahiri mkubwa wa uongozi na matokeo yake Bunge hili litaendelea kumkumbuka.

7. ***Mheshimiwa Spika***, naomba nikupongeze wewe binafsi na Naibu Spika, kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa umakini, busara na hekima kubwa. Nawapongeza pia Wenyeviti wa Bunge kwa ustadi wa kazi wanayoifanya ya kuliongoza Bunge letu, hakika wamekuwa msaada mkubwa sana katika uendeshaji wa Bunge kwa ujumla.

8. ***Mheshimiwa Spika***, Nawapongeza pia Mawaziri wote wa Serikali ya Awamu ya Tano kwa mafanikio makubwa wanayoendelea kuyaleta kwa wananchi wa Tanzania kupitia usimamizi wao mahiri wa utekelezaji wa llani ya Uchaguzi ya CCM na Dira ya Maendeleo ya Mwaka 2025. Kipekee napenda kumshukuru Waziri mwenzangu katika Ofisi ya Rais, Mheshimiwa Selemani Jafo (Mb) anayeshughulika na

Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa ushirikiano mkubwa anaonipa pamoja na Viongozi wenzake wa Ofisi ya Rais TAMISEMI maana shughuli zetu zinategemeana sana.

9. *Mheshimiwa Spika*, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mhe. Jumanne Mtaturu (Mb.) kwa kuchaguliwa bila kupingwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Singida Mashariki katika uchaguzi mdogo uliofanyika. Vile vile, kwa masikitiko makubwa natoa pole kwa msiba wa Mhe. Rashid Ajali Akbar aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Newala Vijijini uliotokea tarehe 15 Januari, 2020. Tunaomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi, Amina!

10. *Mheshimiwa Spika*, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mhe. George Boniface Simbachawene (Mbunge wa Kibakwe) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mbunge wa Ilala) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia Muungano na Mazingira. Nawatachia mafanikio katika nafasi hizi walizopewa na Mheshimiwa Rais.

11. *Mheshimiwa Spika*, nawashukuru Balozi Mhandisi John William Kijazi, Katibu Mkuu Kiongozi; Dkt Moses Kusiluka, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Ikulu; Dkt. Laurean J. Ndumbaro, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Dkt Francis Michael, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti

ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Makamishna, Watendaji Wakuu wa Taasisi; Wakurugenzi na Watumishi wote wa Ofisi ya Rais Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kazi nzuri wanazozifanya katika kutekeleza majukumu yanayoiwezesha Ofisi kufikia malengo yake, ikiwa ni pamoja na kukamilisha Hotuba hii kwa wakati. Aidha, napenda kuwashukuru waajiri na watumishi wote wa Umma kwa kutekeleza wajibu wao kwa ufanisi, uzalendo na imani yao kwa uongozi wa Serikali ya Awamu ya Tano ambao umeiwezesha Serikali kutekeleza majukumu yake ya kuwahudumia wananchi.

12. *Mheshimiwa Spika*, kwa namna ya pekee napenda kuzishukuru Nchi Wahisani na Washirika wa Maendeleo ambao wamechangia jitihada zetu za kuleta maendeleo kwa wananchi. Hivyo, nachukua fursa hii kuwashukuru na kuwataja wachache ambao ni:- Jamhuri ya Watu wa China, Japan, Uingereza, India, Jamhuri ya Korea, Canada, Marekani, Sweden, Australia, Umoja wa Ulaya, Denmark, Norway, Uhlanzi, Finland, Uswisi, Italia, Malaysia, Misri, Singapore, Cuba, Thailand na Ireland. Vile vile, nayashukuru Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa ambayo ni: Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia (WB), OFID-OPEC Fund for International Development, DfID, KOICA, GIZ, USAID, SIDA, UNDP, Jumuiya ya Madola, DANIDA, JICA, UNICEF, ILO, WFP, UN Women, Global Fund, Mfuko wa Fedha wa

Kimataifa (IMF) na Taasisi ya Bill and Melinda Gates Foundation.

13. *Mheshimiwa Spika*, natumia fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Newala Mjini kwa kuendelea kunipa ushirikiano wakati wote ninapoendelea kuwawakilisha. Ahadi yangu kwao ni kutowaangusha katika kulijenga na kuliletea maendeleo Jimbo letu. Vile vile, naishukuru familia yangu kwa ushirikiano wanaonipa na kwa maombi yao wakati wote ninapotekeleza majukumu ya Kitaifa.

14. *Mheshimiwa Spika*, kwa masikitiko makubwa natoa pole kwa Watanzania wenzetu, Viongozi na Watumishi wa Umma waliopotelewa na ndugu zao kutokana na majanga mbalimbali yaliyotokea katika kipindi hiki. Sote tumeshuhudia majanga yaliyoikumba nchi yetu ikiwemo ajali ya lori la mafuta iliyotokea mwezi Agosti 2019 Mjini Morogoro ambayo ililetu simanzi kubwa katika Taifa letu. Ajali hiyo ilisababisha vifo vya watu takriban 104 na wengine kuachwa na ulemavu. Majanga mengine yaliyotokea ni: ajali ya Treni ya Uokoaji na Kiberenge iliyotokea mwezi Machi, 2020 katika reli inayotoka Ruvu Junction ambayo ilisababisha vifo vya watumishi watano na kujeruhi mtumishi mmoja; vifo vya wanajeshi wetu 10 wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania vilivyotokea mwezi Februari 2020 Msata, mkoani Pwani wakati wakishiriki mazoezi ya Kijeshi na Askari watatu wa Jeshi la Polisi waliofariki

kwa ajali ya gari mkoani Njombe. Vile vile, athari za mvua kubwa zinazoendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali nchini ambazo zimesababisha vifo na wengine kubaki majeruhi. Hali kadhalika, mvua hizi zimeleta uharibifu mkubwa wa mali na miundombinu ya barabara na madaraja. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awaponye waliojeruhiwa ili waendelee kujenga taifa letu na kwa waliofariki dunia, Mwenyezi mungu aziweke roho zao mahala pema peponi.

15. *Mheshimiwa Spika*, tunatambua kwamba Dunia kwa sasa imekumbwa na mlipuko wa ugonjwa unaosababishwa na virusi vya Corona - COVID 19. Ugonjwa huu umeshababisha vifo katika nchi mbali mbali na wagonjwa wengine wanaendelea kupata matibabu. COVID 19 iliripotiwa kuingia nchini mwetu mwezi Machi, 2020 ambapo Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto wameendelea kuelekeza na kuchukua hatua mbali mbali ili kukabiliana na janga hili. Nikiwa Waziri mwenye dhamana na Utumishi wa Umma, natoa rai kwa watumishi wote nchini kufuata na kuzingatia maelekezo yanayotolewa na Viongozi pamoja na Wataalam wa afya ili kujikinga na ugonjwa huu na kuzuia kusambaa kwa maambukizi ya virusi vya Corona. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awaponye wote waliothibitika kupatwa na ugonjwa huu na pia atukinge na janga hili.

16. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka wa Fedha 2019/20 tuliwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu maombi ya fedha kwa ajili ya kutekeleza mipango kazi inayowezesha Ofisi yangu kwa mazingatio ya kisera na kimkakati. Kwa mara nyingine tupo mbele ya Bunge lako tukufu ili kutoa Taarifa ya Utekelezaji wa shughuli tulizoombea fedha kwa Mwaka wa Fedha 2019/20 pamoja na kuwasilisha mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/21.

A. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MWAKA WA FEDHA 2019/20

17. *Mheshimiwa Spika*, utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/20 ulizingatia, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21) na llani ya Uchaguzi ya Chama Tawala ya Mwaka 2015 pamoja na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025. Shughuli zilizotekelawa na kila taasisi ni kama ifuatavyo:-

OFISI YA RAIS, IKULU NA TAASISI ZAKE

18. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka wa Fedha 2019/20, Fungu: 20 Ofisi ya Rais, Ikulu iliidhinishiwa **Shilingi 23,144,913,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Machi, 2020 **Shilingi 17,044,246,000** zilipokelewa na kutumika.

19. *Mheshimiwa Spika*, ili kutekeleza majukumu yake, katika Mwaka wa Fedha 2019/20, Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri (Fungu 30) inayojumuisha Taasisi zilizo chini ya Ikulu, iliidhinishiwa **Shilingi 564,312,423,717**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 410,123,039,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 154,189,384,717** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2020, **Shilingi 429,371,669,447.57** zilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo **Shilingi 335,850,018,390.56** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 93,521,588,057.01** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Yafuatayo ni maelezo kwa kila Taasisi:-

a. OFISI YA RAIS - IKULU

20. *Mheshimiwa Spika*, Ofisi ya Rais, Ikulu imeendelea kuongoza, kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali. Katika kipindi cha mwezi Julai, 2019 hadi Machi, 2020, kazi zifuatazo zilitikelezwa:-

- (i) Huduma ziliendelea kutolewa kwa Mheshimiwa Rais na familia yake;
- (ii) Ushauri umetolewa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu ratiba ya kila siku;
- (iii) Ushauri umetolewa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika masuala ya Siasa, Uchumi, Jamii, Sheria, Diplomasia,

Mawasiliano na Habari, Uhusiano wa Kikanda, Kimataifa na ushauri mwingine kwa lengo la kumsaidia Rais kufanya na kufikia maamuzi sahihi;

- (iv) Mikutano 31 ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ilifanyika, ambapo nyaraka 68 zilichambuliwa. Mikutano 15 ya Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu (IMTC) ilifanyika na nyaraka 35 zilichambuliwa na ushauri kutolewa. Mikutano 15 ya kazi ya Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu (IMTC) ilifanyika ambapo mada 45 ziliwasilishwa na kujadiliwa. Mikutano sita (6) ya Baraza la Mawaziri ilifanyika ambapo nyaraka 29 zilijadiliwa na kufanyiwa maamuzi. Aidha, mikutano mitatu (3) ya Kamati ya Katiba na Bunge ya Baraza la Mawaziri ilifanyika ambapo miswada 12 ilijadiliwa;
- (v) Kumbukumbu za Mikutano ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu na Baraza la Mawaziri ziliandaliwa na kusambazwa kwa wakati kwa wahusika. Aidha, ufuatiliaji na tathmini ya Maamuzi ya Baraza la Mawaziri ulifanyika na taarifa ya utekelezaji wake iliandaliwa;
- (vi) Ziara ya Maafisa wa Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri kutembelea migodi ya madini na masoko ya madini katika Mikoa ya Arusha, Shinyanga, Geita, Mwanza na Mara ilifanyika

tarehe 19 – 30 Februari, 2020 ili kuona hali halisi ya utekelezaji na kushauri ipasavyo;

- (vii) Ziara ya Maafisa wa Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati ya Ujenzi wa Reli kwa Kiwango cha Kimataifa (SGR) na Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere ilifanyika tarehe 2 – 4 Machi, 2020;
- (viii) Uratibu wa utekelezaji wa Programu ya Kujenga Uwezo wa taasisi za Serikali Kupambana na Rushwa (BSAAT) inayotekelzwa na taasisi nufaika 9 nchini ulifanyika;
- (ix) Ufutiliaji wa utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu (NACSAP III) umefanyika kwa kupitia Taarifa za utekelezaji kutoka kwenye Wizara, Wakala, Idara za Serikali Zinazojitegemea, na Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- (x) Elimu kwa umma kuhusu Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa imetolewa kwa wawakilishi wa Wamiliki wa Vyombo vya Habari, Viongozi wa Madhehebu ya Dini na katika Mkutano wa Mwaka wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa Jijini Dar es salaam, Mwanza na Dodoma;
- (xi) Mafunzo kuhusu maudhui na usimamizi wa utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa, Awamu ya Tatu yalitolewa kwa

Viongozi na Wajumbe wa Kamati ya Kudhibiti Uadilifu kwa Vyuo Vikuu vya Sokoine, Mzumbe na Dodoma, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Mamlaka ya Mawasiliano, Mamlaka ya Usimamizi wa Huduma za Bima, Watumishi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Shirika la Umeme Tanzania;

- (xii) Mafunzo ya majaribio ya mfumo wa kieletroniki wa Taarifa za Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa yametolewa kwa wawakilishi wa Wajumbe wa Kamati za Kudhibiti Uadilifu katika Wizara, Mikoa na Halmashauri za Mwanza na Dodoma;
- (xiii) Rufaa 151 za Watumishi wa Umma, Mamlaka ya Nidhamu na Waajiri zilichambuliwa na kutolewa uamuzi na Rais na Katibu Mkuu Kiongozi ambapo wahusika walijulishwa. Aidha, malalamiko 459 ya Watumishi wa Umma na wananchi wengine yalichambuliwa na kutolewa maelekezo;
- (xiv) Ufuatiliaji wa uzingatiaji wa sheria na maelekezo yanayotolewa na Katibu Mkuu Kiongozi na Mkuu wa Utumishi wa Umma ulifanyika katika mikoa ya Kagera, Geita na Dar es Salaam;
- (xv) Majibu na ushahidi kwenye kesi za madai 16 zinazohusu watumishi wa Umma na wananchi wengine zilizoko Mahakama Kuu zinazopinga uamuzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania au Katibu Mkuu Kiongozi yalitolewa kwa kushirikiana na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali;

- (xvi) Mikutano mitatu (3) ya uratibu na uendeshaji wa maboresho ilifanyika kujadili mafanikio, changamoto na mipango ya baadae ya maboresho; na
- (xvii) Ujenzi na ukarabati wa majengo katika Ikulu ya Chamwino umefanyika.

b.TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA (TAKUKURU)

21. *Mheshimiwa Spika*, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329. Majukumu hayo ni pamoja na kuelimisha Umma kuhusu athari za rushwa, kuchunguza tuhuma za makosa ya rushwa, kuwafikisha watuhumiwa mbele ya vyombo vyia sheria na kuishauri Serikali kuhusu masuala mbalimbali ya mapambano dhidi ya rushwa.

22. *Mheshimiwa Spika*, Juhudi zinazochukuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli katika kukabiliana na vitendo vyia rushwa nchini zimeleta mafanikio makubwa kwa kuongeza nidhamu, uadilifu na uwajibikaji katika nyanja mbalimbali zikiwemo za utumishi wa umma, biashara,

ukusanyaji mapato na matumizi ya fedha za umma. Mafanikio haya yameijengea Serikali msingi/uwezo imara wa kukuza uchumi na kuongeza kasi ya utoaji huduma za kijamii kwa wananchi.

23. *Mheshimiwa Spika*, Matokeo ya utafiti uliofanywa na taasisi mbalimbali za kimataifa na za kitaifa kuhusu hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kupambana na rushwa nchini zimedhihirisha kuwa Tanzania inafanya vizuri katika kudhibiti vitendo vyatrushwa na ufisadi nchini.

24. *Mheshimiwa Spika*, Kiashiria cha Corruption Perception Index (CPI) cha Taasisi ya Kimataifa ya Transparency International ambacho kinapima hali ya rushwa kwa kutumia mzani wa 0-100 ambapo nchi inayopata alama (0) ndiyo imekithiri kwa rushwa na inayopata alama 100 ndiyo inafanya vizuri zaidi, kimeonesha kuwa katika utafiti wa mwaka 2019, kuwa Tanzania imeendelea kufanya vizuri kwa kufikia kiwango cha asilimia 37 na kushika nafasi ya 96 kati ya nchi 180 duniani ikiwa ni kupanda kwa nafasi 23 ikilinganishwa na kiwango cha asilimia 30 katika nafasi ya 119 ya mwaka 2015. Aidha, kwa kutumia kiashiria cha Mo Ibrahim taarifa ya mwaka 2018, inaonesha kuwa kwa kipindi cha miaka kumi kuanzia mwaka 2008 hadi 2017, Tanzania ilipiga hatua katika nyanja ya Utawala Bora kwa kupata asilimia 58.5 na kuwa nchi ya 14 kati ya nchi 54 za Afrika.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo Tanzania ni miongoni mwa nchi sita za Afrika zinazopiga hatua katika nyanja ya uwazi na uwajibikaji mwaka hadi mwaka.

25. *Mheshimiwa Spika*, Utafiti uliofanywa na AFROBAROMETER mwaka 2014 ulionesha kuwa asilimia 66 ya waliohojiwa walisema kuwa kiwango cha rushwa kimeongezeka. Hata hivyo, matokeo ya utafiti uliofanyika wa mwaka 2017 yanaonesha kuwa asilimia 72 ya waliohojiwa walisema kuwa kiwango cha rushwa kimepungua. Aidha, matokeo ya utafiti uliofanywa na TWaweza mwaka 2017 nao umebainisha kuwa asilimia 85 ya wananchi waliohojiwa walieleza kuwa rushwa imepungua ukilinganisha na asilimia 11 ya waliohojiwa mwaka 2014.

26. *Mheshimiwa Spika*, Matokeo ya utafiti uliofanywa na Transparency International's Global Corruption Barometer for Africa na ripoti yake kutolewa Julai, 2019 juu ya mtazamo na uzoefu wa wananchi kuhusu rushwa, katika kipengele cha juhudi za Serikali katika mapambano dhidi ya rushwa yanaonesha Tanzania imefanya vizuri kwa kuwa ya kwanza kati ya nchi 35 za Afrika zilizofanyiwa utafiti.

27. *Mheshimiwa Spika*, Aidha, matokeo ya utafiti uliofanywa mwaka 2019 na World Economic Forum kuhusu ufanisi katika matumizi ya umma (efficiency of Government spending) yamebainisha kuwa Tanzania imeshika nafasi ya 28 kati ya nchi 136 duniani zilizofanyiwa utafiti huo.

28. *Mheshimiwa Spika*, Katika kipindi cha mwezi Julai, 2019 hadi Machi, 2020 Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

- (i) Uchunguzi wa majalada 183 ulikamilika na kuwasilishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kuombewa kibali ambapo Majalada 47 yalipata kibali cha kuwafikisha watuhumiwa mahakamani. Aidha, majalada mengine yanaendelea kufanyiwa kazi;
- (ii) Kesi mpya 352 zilifunguliwa mahakamani katika kipindi hiki na kufanya jumla ya kesi zilizoendeshwa mahakamani kufikia 762. Katika kipindi hiki, kesi 339 ziliamuliwa mahakamani ambapo kesi 143 watuhumiwa wake waliachiwa huru na kesi 196 watuhumiwa wake walipatikana na hatia na kuhukumiwa kifungo au kulipa faini. Kesi 649 zinaendelea mahakamani;
- (iii) **Shilingi bilioni 50.8** zimeokolewa kutokana na operesheni mbalimbali za uchunguzi na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo unaofanyika kote nchini ambapo **Shilingi bilioni 6.7** ni fedha taslimu

zilizorejeshwa Serikalini, **Shilingi bilioni 11.2** ni thamani ya mali zilizotaifishwa ambazo ni nyumba tatu (3) na viwanja vinne (4), **Shilingi bilioni 30.0** ziliokolewa baada ya uchunguzi kufanyika na kubaini mzabuni aliongeza bei kwenye huduma aliyotoa serikalini na **Shilingi bilioni 2.9** zilidhibitiwa au kurejeshwa kwa wananchi. Aidha, kiasi cha fedha na mali zilizowekewa zui o kusubiria kukamilika kwa taratibu za kisheria za utaifishaji ni: **Shilingi bilioni 7.0; dola za kimarekani milioni 5.26;** magari 14 yeny e thamani ya **Shilingi milioni 635,** nyumba 14 zeny e thamani ya **Shilingi bilioni 13.0** na nyumba moja (1) yeny e thamani ya **Dola za Marekani 410,000;**

- (iv) Utafiti weny e lengo la kuimarisha mifumo ya udhibiti wa mianya ya rushwa umefanyika katika maeneo ya ukusanyaji mapato unaofanywa na Halmashauri, Ukadiriaji wa kodi unaofanywa na TRA na manunu zi ya umma. Matokeo na mapendelekezo ya kuziba mianya ya rushwa katika maeneo haya yamewasilishwa kwa mamlaka husika ili hatua stahiki zichukuliwe;
- (v) Kazi 275 za uchambuzi wa mifumo zilifanyika katika sekta mbalimbali zikiwemo Vyama vya Ushirika wa masoko ya mazao ya kilimo (AMCOS), uwekezaji na mapato, ambapo kutokana na kazi hizo, hatua zimechukuliwa

ikiwemo kuanzisha uchunguzi, kutoa elimu kwa umma na kushauri mamlaka husika namna ya kudhibiti mianya ya rushwa katika vyama hivyo;

- (vi) Ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za umma katika Miradi ya maendeleo nchini umefanyika ili kuhakikisha thamani halisi ya fedha inapatikana. Miradi 244 ya maendeleo yenyе thamani ya **Shilingi bilioni 9,860** katika sekta za kipaumbele za Afya, Elimu, Maji, Ujenzi na Nishati ilifuatiliwa. Kati ya miradi hiyo, miradi 34 yenyе thamani ya **Shilingi bilioni 8.90** ilionekana kuwa na kasoro mbalimbali na inaendelea kufanyiwa uchunguzi;
- (vii) Utafiti wa kitaifa wa hali ya rushwa na utawala bora (National Governance and Corruption Survey) unaendelea. Utafiti huu unatarajiwa kukusanya taarifa kuhusu kiwango cha rushwa, aina za rushwa na tabia/mbinu mpya za vitendo vya rushwa kwa lengo la kuisaidia Serikali kuweka msingi wa kisayansi ili kuendelea kukabiliana na tatizo la rushwa nchini;
- (viii) Warsha/vikao 294 vya Wadau kujadili matokeo ya kazi za utafiti na uchambuzi wa mifumo kwa lengo la kuweka mikakati ya kudhibiti rushwa vilifanyika katika maeneo ya ujenzi wa hospitali za wilaya, usambazaji wa umeme vijijini na sekta ya Elimu (fedha za Ruzuku kwa shule za msingi);

- (ix) Kazi 196 za ufuatiliaji wa utekelezaji wa maazimio yatokanayo na mapendekezo ya uchambuzi wa mifumo zilifanyika ili kuziba mianya ya rushwa katika maeneo ya ukusanyaji wa mapato kwa kutumia POS (Point of Sales) na EFDs; udhibiti wa rushwa katika ukusanyaji wa kodi ya majengo; miradi ya maji; huduma za utoaji Hati za Kusafiria na ukusanyaji wa mapato katika Jiji la Dar es Salaam;
- (x) Elimu kuhusu athari za rushwa na juhudzi za Serikali za kuidhibiti ili kupata uungwaji mkono ilitolewa kwa umma kupitia njia mbalimbali zikiwemo semina 3,296, mikutano ya hadhara/mijadala 3,186, vipindi vya redio na televisheni 511, maonesho 291 na taarifa kwa umma 179 zilitolewa kupitia vyombo vya habari. Aidha, habari/makala 370 ziliandaliwa kwa ajili ya wavuti na jarida la TAKUKURU na matangazo manne yaliandaliwa kwa ajili ya kuelimisha umma;
- (xi) Elimu kuhusu rushwa ilitolewa kwa vijana walio shuleni na vyuoni ambapo Klabu za wapinga rushwa 5,418 ziliimarishwa ili kujenga kizazi cha vijana wenye maadili na wanaochukia rushwa;
- (xii) Kampeni ya UTATU inayoshirikisha TAKUKURU, POLISI na Wadau ilizinduliwa ikiwa na mfumo wa kielektroniki wa kunasa na kuripoti matukio

ya vitendo vya rushwa barabarani na sehemu nyingine;

- (xiii) TAKUKURU imepokea malalamiko na taarifa kutoka kwa wananchi saa 24 kwa siku ambapo wananchi 166,643 wameweza kuifikia TAKUKURU kwa simu namba 113 ambapo walipata fursa ya kutoa maoni, ushauri, kuuliza maswali na kutoa taarifa za vitendo vya rushwa;
- (xiv) Kampeni ya “Vunja Ukimya” inayolenga kudhibiti rushwa ya ngono iliendeshwa katika mikoa yote. Lengo kubwa likiwa ni kuwahamasisha wanaokumbana na vitendo hivyo na wananchi kwa ujumla kutoa taarifa TAKUKURU ili hatua dhidi ya wahusika zichukuliwe;
- (xv) Elimu kwa umma imetolewa kupitia vyombo vya habari na mitando ya kijamii kubeba agenda ya mapambano dhidi ya rushwa ambapo jumla ya matangazo 19 yaliandaliwa na kusambazwa kwa njia ya “Whatsup”, taarifa mbalimbali zimeendelea kutolewa kwenye mitando ya “Twitter”, “WhatsApp” na “Instagram”. Aidha, TAKUKURU imepata usajili wa TAKUKURU Online TV ili kuwashirikisha wananchi wengi kwa gharama nafuu;
- (xvi) Mfumo wa TEHAMA ndani ya TAKUKURU umeimarishwa kwa kuunganisha Ofisi za wilaya 58 kwenye mtando wa taasisi na kuboresha njia

za mawasiliano katika mikoa 17 kwa lengo la kurahisisha mtiririko mzuri wa majalada, takwimu na mawasiliano kutoka ngazi za Wilaya, Mikoa na Makao Makuu;

- (xvii) Huduma za TAKUKURU zimesogezwa kwa wananchi kwa kufungua Ofisi kwenye Wilaya mpya 21 na hivyo kufanya Takukuru kuwa na Ofisi katika Mikoa na Wilaya zote Tanzania Bara. Ofisi hizi zimepatiwa watumishi na vitendea kazi ikiwemo magari; na
- (xviii) Watumishi 234 walipatiwa mafunzo ili kuwajengea uwezo wa kumudu majukumu kwa ufanisi.

c. TAASISI YA UONGOZI

29. *Mheshimiwa Spika*, Taasisi ya UONGOZI imeendelea kusimamia malengo yake ya kuwa Kituo cha Utaalam wa Hali ya Juu cha kuendeleza Viongozi Barani Afrika kwa kuanzia na Tanzania, Ukanda wa Afrika Mashariki na hatimaye Afrika kwa ujumla. Walengwa ni Viongozi Waandamizi waliopo na wanaojitokeza wakiwemo wanasiasa, watumishi wa Serikali na Mahakama.

30. *Mheshimiwa Spika*, Katika kipindi cha mwezi Julai, 2019 hadi Machi, 2020 shughuli zifuatazo zilitaktelezwa:-

- (i) Programu ya Stashahada ya Uzamili ya Uongozi iliendelea kutekelezwa. Stashahada hii inalenga kuwajengea viongozi uwezo wa kufanya maamuzi ya kimkakati, kusimamia rasilimaliwatu na rasilimali nyingine na kujenga sifa binafsi za kiongozi. Stashahada hii yenye moduli 10 inatekelezwa kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Aalto kilichoko Helsinki, nchini Finland. Katika kipindi hiki, awamu ya tatu ya mafunzo inayojumuisha Maafisa Waandamizi 33 kutoka Wizara, Taasisi na Mashirika ya Umma iliendelea kutekelezwa;
- (ii) Viongozi wa Umma 628 wamepata mafunzo ya muda mfupi kupitia kozi 17 kwa lengo la kuimarisha utendaji na kupanua uelewa katika masuala ya kiuongozi. Kozi zilizotolewa zilihusu maeneo ya Uongozi; Uongozi wa Kimkakati; Uongozi Wenye Maadili; Mapambano Dhidi ya Rushwa, Uongozi Binafsi na Akili Hisia, Matumizi Sahihi ya Muda kama rasilimali ya umma; Uongozi na Usimamizi wa Mabadiliko ndani ya taasisi na Usimamizi wa Sekta Binafsi;

- (iii) Kwa kushirikiana na taasisi za ndani na nje ya nchi, makongamano matano (5) ya Kimataifa, Kikanda na Kitaifa yalifanyika kwa lengo la kukutanisha viongozi ili kubadilishana taarifa, maarifa na uzoefu na kuwaongezea uelewa wa masuala ya Uongozi na Maendeleo Endelevu. Jumla ya viongozi 1,479 walishiriki kutoka Tanzania na nchi mbalimbali ndani na nje ya Afrika. Mikutano ifuatayo ilifanyika:-
- (a) Kongamano la Kikanda la Viongozi wa Afrika kuhusu “Usimamizi bora wa Rasilimali kwa Maendeleo Endelevu Barani Afrika”, lilifanyika tarehe 26 na 27 Julai, 2019. Kongamano liliandaliwa kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Mstaafu Benjamin William Mkapa. Kongamano lilihudhuriwa na Viongozi 161 kutoka nchi 21, wakiwemo Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Marais Wastaafu kutoka Tanzania, Afrika ya Kusini, Nigeria, Madagascar, na Somalia; Wakuu wa Taasisi za Kimataifa na Kikanda za FAO, UNEP, UNU-Institute for Natural Resources, SADC, EAC, AfDB, AGRA na WWF, wafanyabiashara maarufu, Wakuu wa Taasisi za Kiraia, na wanataaluma;

- (b) Kongamano la Kikanda juu ya “Kuimarisha Ushirikiano ndani ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC)” lilifanyika ambapo mada kuu ilitolewa na Mhe. Benjamin William Mkapa, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania. Kongamano liliandaliwa kwa kushirikiana na Sekretarieti ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kuhudhuriwa na Viongozi 515 kutoka nchi za SADC akiwemo Mhe. Netumbo Nandi-Ndaitwah, Naibu Makamu wa Rais na Waziri wa Mahusiano ya Kimataifa wa Namibia, Mhe. Harrison Mwakyembe, aliyemwakilisha Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Dkt. Stergomena Tax, Katibu Mtendaji wa Sekretarieti ya SADC;
- (c) Kongamano la kitaifa kuhusu “Usimamizi wa Misitu kwa Lengo la Kukuza Rasilimali Maji” lilifanyika kama sehemu ya Jukwaa la Maendeleo Endelevu. Kongamano lilifunguliwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye pia ni mlezi wa Jukwaa. Kongamano hili lilihudhuriwa na viongozi 99 kutoka Wizara na Idara za Serikali, Asasi za kiraia, na Sekta Binafsi;

- (d) Kongamano la Kumbukizi ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere juu ya: "Tanzania Miaka 20 baada ya Mwalimu" liliandaliwa kwa kushirikiana na Kigoda cha Mwalimu Nyerere na kuhudhuriwa na washiriki 585, wakiwemo viongozi waliopo madarakani, wastaafu na wanafunzi wa Vyuo na Sekondari; na
- (e) Kongamano la Kitaifa kuhusu "Ushiriki wa Watanzania katika Miradi ya Kimkakati: Mafanikio, Fursa na Changamoto" lilifanyika kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Uvezeshaji Wananchi Kiuchumi. Kongamano hili liliambatana na uzinduzi wa Miongozo ya Kitaifa na Kisekta ya Ushiriki wa Watanzania na uzinduzi wa Tovuti ya Miradi ya Kimkakati ambapo Washiriki 175 walihudhuria kongamano hilo.
- (iv) Vipindi vitano (5) vya mahojiano na viongozi waandamizi na wataalam wa masuala ya Uongozi na Maendeleo Endelevu viliandaliwa na kurushwa kwenye runinga na kuwekwa kwenye tovuti ya Taasisi ya UONGOZI na mitandao ya kijamii kwa lengo la kubadilishana taarifa, maarifa na uzoefu. Vipindi hivi vinaonekana Bara zima la Afrika;

- (v) Kwa kushirikiana na Taasisi ya Umoja wa Mataifa; UNU-WIDER, iliyoko Finland tafiti 22 zinafanyika kwenye maeneo ya uchumi wa Viwanda, Uchumi Mpana, Fedha, Usimamizi wa Mikopo endelevu, pamoja na maeneo mengine;
- (vi) Kitabu kinachoelezea maisha ya Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu Mhe. Benjamin William Mkapa kilichapishwa na kuzinduliwa tarehe 12 Novemba, 2019 na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Uzinduzi huu ulihudhuriwa na washiriki 545 wakiwemo marais wastaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na viongozi wengine kutoka serikalini na mashirika mbalimbali. Aidha, chapisho la maisha ya Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili Mhe. Ali Hassan Mwinyi linaendelea kuandaliwa; na
- (vii) Chapisho kuhusu masuala ya Maendeleo Endelevu lilitolewa.

d. MPANGO WA KURASIMISHA RASILIMALI NA BIASHARA ZA WANYONGE TANZANIA (MKURABITA)

31. *Mheshimiwa Spika*, Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) umeendelea kutekeleza jukumu la kuandaa na kusimamia mfumo wa Kitaifa wa umiliki wa rasilimali na uendeshaji wa Biashara nchini unaotambulika na kukubalika kisheria. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, MKURABITA imetekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Wakulima 180 na viongozi 22 wa Vyama vya wakulima wamejengewa uwezo wa kutumia Hati za Haki Miliki za Kimila kupata Mitaji katika Benki na Taasisi zingine za Fedha katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa katika Vijiji vya Mvumi na Magubike. Aidha, mafunzo yaliyotolewa yamewezesha Wakulima 48 kufungua akaunti katika benki;
- (ii) Huduma za Urasimishaji wa Biashara zimesogezwa kwa wananchi kwa kuanzisha Vituo vya Huduma kwa Pamoja katika Manispaa ya Tabora na Mji wa Babati ambapo huduma muhimu za utoaji leseni za biashara, utoaji wa Namba ya Utambulisho wa Mlipa kodi (TIN) kuitia TRA, usajili wa jina la biashara kuitia BRELA, huduma za benki na mifuko ya hifadhi ya jamii zinapatikana sehemu moja. Aidha,

wafanyabiashara 1,529 wamepata mafunzo ya urasimishaji na uendeshaji wa biashara. Katika kipindi husika Vituo vimesajili biashara 396 na wafanyabiashara 420 wamefungua akaunti katika benki kwa ajili ya kuweka akiba na kukopa fedha ili kujiongezea mitaji. Uwekaji wa huduma za Urasimishaji wa Biashara kwa wananchi kwa kuanzisha vituo katika Halmashauri ya Manispaa ya Nyamagana pamoja na Miji ya Kahama na Songea umeanza;

- (iii) Zoezi la Urasimishaji wa Ardhi Mijini kwa dhana ya Mfuko Endelevu wa Wilaya limeanza kwa kufanya utambuzi wa milki 200 kati ya 1,000 zilizopangwa katika Halmashauri ya Manispaa ya Iringa;
- (iv) Hati za Haki Milki za Kimila 159 katika kijiji cha Inzomvu kilichopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa zimetolewa;
- (v) Elimu kwa umma kuhusu utekelezaji wa shughuli za urasimishaji imetolewa kupitia vipindi 14 vya redio na runinga za TBC. Maudhui ya vipindi yalihusu maeneo yaliyofanyiwa urasimishaji katika Halmashauri za Wilaya za Mbarali, Kilombero, Kilosa, Urambo, Misungwi, Manispaa za Ilala, Mtwara, Singida, Morogoro, Jiji la Tanga, na Halmashauri za Miji ya Njombe, Geita na Bariadi; na

- (vi) Ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa shughuli za urasimishaji umefanyika katika Halmashauri ya Wilaya ya Itigi katika Vijiji vya Sanjaranda na Kitopeni.

e. MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII (TASAF)

32. *Mheshimiwa Spika*, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii umeendelea kutekeleza Awamu ya Tatu ya TASAF kwa kuyapa kipaumbele maeneo ya Ukuzaji wa uchumi na kupunguza umaskini wa kipato; Kuinua ubora wa maisha na ustawi wa jamii; na Utawala bora na uwajibikaji. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Mfuko wa Maendeleo Jamii (TASAF) umetekeliza kazi zifuatazo:-

- (i) Ruzuku ya **Shilingi bilioni 35.6** ilihawilishwa kwa kaya maskini zilizopo kwenye Mpango ambazo zina watu 4,920,344 kwa Tanzania Bara na Zanzibar katika Vijiji/Mitaa/Shehia 9,867. Kaya hizo zimeweza kupata ruzuku hiyo kwa masharti ya lishe, afya na elimu;
- (ii) Mpango wa kutoa ajira za muda umetekeliza miradi 1,521 kutoka katika Vijiji, Mitaa na Shehia zipatazo 1,212 ambapo kaya za walengwa 161,416 zilipata ajira za muda katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 42 na Wilaya zote za Zanzibar. Miradi hiyo ina thamani ya **Shilingi bilioni 6.4.** Miradi iliyotekeliza ni pamoja na

ujenzi na ukarabati wa malambo ya maji, uanzishaji wa vitalu vya miche ya miti, uchimbaji wa visima vifupi, uboreshaji wa barabara, uhifadhi wa vyanzo vya maji na hifadhi ya mazingira;

- (iii) Miradi 119 ya miundombinu ya elimu, afya na maji yenyе thamani ya **Shilingi bilioni 11.23** imetekelезwa katika Halmashauri 11 za Mikoa ya Arusha, Njombe, Tanga, Mtwara na Tabora. Aidha, mafunzo kuhusu taratibu za utekelezaji na usimamizi wa miradi katika maeneo husika yalitolewa kwa wawezeshaji wa ngazi ya Halmashauri na wajumbe wa Kamati za Usimamizi za Jamii;
- (iv) Mfumo wa malipo kwa Walengwa kwa njia za kielektroniki (kupitia mitandao ya simu na Benki) umeandaliwa na majaribio yamefanyika katika Mamlaka ya Maeneo ya utekelezaji 16 ambayo ni; Jiji la Arusha, Manispaa ya Ilala, Manispaa ya Kinondoni, Manispaa ya Temeke, Halmashauri ya Bahi, Mpanda Mji, Halmashauri ya Siha, Halmashauri ya Kilwa, Halmashauri ya Bagamoyo, Halmashauri ya Kisarawe, Manispaa ya Kigoma – Ujiji, Halmashauri ya Mkuranga, Manispaa ya Songea, Halmashauri ya Urambo, Halmashauri ya Muheza, na Halmashauri zote za Unguja kwa upande wa Zanzibar. Hadi kufikia Februari, 2020 Walengwa 55,087 walinufaika na

Shilingi bilioni 2.14 zimelipwa kwa kutumia njia hiyo;

- (v) Vikundi 22,303 vya Kuweka Akiba na Kukuza Uchumi wa Kaya vyenye jumla ya walengwa 311,114 vimeundwa katika Mamlaka ya Maeneo ya Utekelezaji 44. Vikundi hivyo vimeweka akiba ya Jumla ya **Shilingi bilioni 2.5** na kukopeshana **Shilingi bilioni 1.6**;
- (vi) Mfumo wa Teknolojia, Habari na Mawasiliano (TEHAMA) wa utunzaji wa kumbukumbu za Walengwa, uendeshaji na utoaji taarifa umeimarishwa. Aidha, Mfumo wa kuwasilisha na kupokea malalamiko umekamilika na umeanza kutumika katika Maeneo yote ya Utekelezaji 161. Mifumo ya TASAF imeunganishwa na mifumo mingine ya kitaifa kama vile NIDA na GePG. Aidha, Kituo cha huduma kwa wateja kimeanzishwa TASAF Makao Makuu na kinafanya kazi;
- (vii) Mfumo wa ukusanyaji takwimu kwa njia ya kielektroniki kwa kutumia kishikwambi (tablet) kwa ajili ya utambuzi wa kaya maskini na ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi umekamilika na kufanyiwa majaribio katika Halmashauri tatu za Mtwara Vijijini, Nanyamba na Siha na kaya 5,219 zilitambuliwa katika vijiji 98. Hadi kufikia Januari 31, 2020, masjala ya walengwa ilikuwa na jumla ya kaya milioni 1.1 zilizoandikishwa

zenye watu milioni 5.2. Aidha, utengenezaji wa kanzidata mpya ya fedha umekamilika na kuanza kufanya kazi;

- (viii) Mapitio ya pamoja ya Timu ya Serikali na Wadau wa Maendeleo kuhusu utekelezaji wa shughuli za Mpango yamefanyika katika vipindi sita vya Julai, 2019 mpaka Februari, 2020. Taarifa zote za mapitio zimeonesha utekelezaji wa Mpango unaendelea vizuri na unawasaidia Walengwa kuondokana na umaskini na kuwajengea uwezo wa kiuchumi na kuwaendeleza watoto katika afya na elimu bora;
- (ix) Mafunzo ya kuwajengea uelewa kuhusu Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini yametolewa kwa Waheshimiwa madiwani 57, Waheshimiwa Masheha 154, Wajumbe wa Kamati za Mradi 220, Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa 30, Wawezeshaji wa Halmashauri 200, Walengwa wa Vikundi vya Kuweka Akiba na Kuwekeza 892 na Wajumbe wa Kamati ya Baraza la Wawakilishi inayosimamia Viongozi Wakuu wa kitaifa Zanzibar 22;
- (x) Mafunzo maalum kuhusu usimamizi wa rasilimali za mpango, ufuatiliaji wa utekelezaji, tathmini za shughuli za mpango, utoaji wa taarifa pamoja na matumizi ya rasilimali ili kuongeza ufanisi na uwajibikaji katika ngazi zote za

utekelezaji wa Mpango yalifanyika kwa wasimamizi wa Mpango katika Mikoa ya Dar es salaam na Pwani pamoja na Unguja kwa upande wa Zanzibar; na

- (xi) Uzinduzi rasmi wa Kipindi cha Pili cha Awamu ya Tatu ya TASAF umefanywa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 17 Februari, 2020, Dar es Salaam. Uzinduzi huo utafuatiwa na utekelezaji wa Mpango baada ya taratibu zote kukamilika.

f. WAKALA WA NDEGE ZA SERIKALI

33. *Mheshimiwa Spika*, Wakala ya Ndege za Serikali ina jukumu la kutoa huduma ya usafiri wa anga kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Viongozi wengine Wakuu wa Kitaifa. Wakala ilianzishwa ili kuboresha huduma na kuimarisha usalama wa usafiri wa ndege kwa viongozi wanaotumia huduma hizo. Aidha, Wakala imeongezewa jukumu lingine la kuratibu kwa niaba ya Serikali, ununuzi wa ndege, kuzikodisha kwa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) na kusimamia mikataba ya ukodishwaji wa ndege hizo.

34. *Mheshimiwa Spika*, Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Wakala wa Ndege za Serikali ilitekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Huduma za usafiri wa anga zimetolewa kwa Viongozi Wakuu wa Kitaifa ambapo jumla ya safari 117 za ndani na tano za nje ya nchi zilifanyika;
- (ii) Wanahewa 34 wamepatiwa mafunzo ya kisheria ya uhuishaji wa leseni zao;
- (iii) Matengenezo madogo ya ndege tatu zinazowahudumia Viongozi Wakuu wa Kitaifa yalifanyika. Aidha, mafuta ya ndege na vipuri vilinunuliwa kadri ya mahitaji;
- (iv) Gharama za bima za ndege pamoja na bima za Wanahewa zililipwa;
- (v) Ukarabati na upanuzi wa karakana za ndege za Serikali umeanza kufanyika;
- (vi) Ndege mbili mpya zilipokelewa ambapo moja ni aina ya Boeing 787- 8 (Dreamliner) na nyingine aina ya De – Havilland (Bombardier) Dash 8 - Q400. Aidha, Wakala imeingia mkataba wa ununuzi wa ndege tatu ambapo moja ni aina ya De - Havilland (Bombardier) Dash 8 - Q400 ambayo inatarajiwa kuwasili nchini mwaka 2020 na mbili ni aina ya Airbus A220 – 300 zinazotarajiwa kuwasili nchini mwaka 2021; na
- (vii) Wakala ya Ndege za Serikali imeingia mikataba miwili ya ukodishaji ndege na Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) na kufanya mikataba iliyosainiwa kufikia nane.

OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

35. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka wa Fedha 2019/20 Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ilitengewa **Shilingi 9,999,946,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 7,382,075,100** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 2,617,870,900** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2020 **Shilingi 4,649,426,253.26** zilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 4,352,256,344.93** ni Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 297,169,908.33** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

36. *Mheshimiwa Spika*, Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

- (i) Malalamiko 113 ya ukiukwaji wa maadili dhidi ya Viongozi wa Umma yalipokelewa na kuchambuliwa. Kati ya malalamiko hayo, malalamiko 58 yalihusu Sheria ya Maadili ya Viongozi na malalamiko 55 hayakuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Uchunguzi kwa malalamiko 15 yanayohusu ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma umekamilika na uchunguzi wa malalamiko 43 unaendelea. Aidha, malalamiko 55 ambayo hayakuhusu ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma walalamikaji walipewa

ushauri na mengine yalielekezwa kwenye mamlaka zinazohusika;

- (ii) Jumla ya Viongozi wa Umma 14,878 ambao ni sawa na asilimia 96 kati ya Viongozi 15,470 wamerejesha Fomu za Tamko la Rasilimali na Madeni kwa kipindi kilichoishia tarehe 31 Desemba, 2019 ikilinganishwa na Viongozi 15,391 waliorejesha kipindi kama hicho mwaka 2018. Viongozi 592 sawa na asilimia 4 ya Viongozi wote bado hawajarejesha Tamko kufikia Februari, 2020;
- (iii) Uhakiki maalum kuhusu Mgongano wa maslahi ulifanyika kwa Waheshimiwa Wabunge na Majaji. Jumla ya Viongozi 203 (Wanaume 120 na wanawake 83) walihojiwa ikiwa ni sawa na asilimia 89 ya viongozi waliotarajiwa. Kati ya viongozi 203 walihojiwa, asilimia 14 walionekana kuwa na viashiria vya mgongano wa maslahi katika mchanganuo ufuatao: asilimia 3 ya viongozi walikuwa ni *hisia ya mgongano wa maslahi*, asilimia 10 walikuwa ni *uwezekano wa kuingia katika mgongano* na asilimia moja ya viongozi walibainika kuwa na *mgongano halisi*. Aidha, uhakiki ulibaini udhaifu wa kimfumo unaoweza kuwaingiza viongozi kwenye migongano ya maslahi wakati wakitekeleza majukumu yao;

- (iv) Elimu kwa umma ilitolewa kwa viongozi wa Umma 2,732, Watumishi wa Umma 5,552 na wananchi 3,545 kuhusu jinsi ya kujiepusha na mgongano wa maslahi na kuishi kwa kuzingatia kiapo cha Ahadi ya Uadilifu. Vipindi 52 vya redio vilitolewa kupitia vyombo mbalimbali vya habari. Aidha, Klabu 32 za Maadili zenyenye wanachama 1,065 zilianzishwa katika shule za Msingi, Sekondari na Vyuo. Klabu 154 zilitembelewa kwa lengo la kukuza na kuendeleza maadili mionganini mwa wanafunzi na wanachama wa klabu. Hadi sasa, Sekretarieti ina zaidi ya klabu 500 za Maadili katika Mikoa mbalimbali nchini zenyenye wanachama 6,000;
- (v) Siku ya Maadili Kitaifa iliadhimishwa Kitaifa Mkoani Dodoma tarehe 10 Desemba, 2019 kwa kushirikiana na Taasisi za Serikali zinazosimamia masuala ya utawala bora, uwajibikaji, haki za binadamu, mapambano dhidi ya rushwa na maadili. Maadhimo ya Siku hii yalihusisha pia mijadala na midahalo ya maadili Kikanda na Kimataifa;
- (vi) Nyenzo za ufuatiliaji na udhibiti wa tatizo la Mgongano wa Maslahi kwa Viongozi wa Umma zimeandaliwa kupitia kikao kazi kilichoshirikisha Taasisi mbalimbali za Umma;
- (vii) Ujenzi wa Ofisi za Sekretarieti ya Maadili Makao Makuu Dodoma umeanza;

- (viii) Mfumo wa Ujazaji Tamko la Rasilimali na Madeni kwa njia ya mtandao umejengwa na kuunganishwa na Mfumo wa Mamlaka za Vitambulisho vya Taifa (NIDA) na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA). Mfumo huu utawezesha Viongozi wa Umma kutuma Tamko la Rasilimali na Madeni kwa njia ya mtandao na kuliwasilisha wakiwa mahali popote kwa kutumia TEHAMA bila kuhitaji kufika katika ofisi za Maadili; na
- (ix) Kanuni za mgongano wa maslahi zimeandaliwa na tayari zimeanza kutumika.

OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA TAASISI ZAKE

a. Menejimenti ya Utumishi wa Umma

37. *Mheshimiwa Spika*, Katika mwaka wa fedha wa 2019/20, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma: Fungu 32 inayojumuisha taasisi zilizo chini yake iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 72,572,322,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa mwaka. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 31,512,322,000** ziliidhinishwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 41,060,000,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2020 **Shilingi 29,437,330,955.89** zilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo **Shilingi 24,666,078,876.93** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 4,771,252,078.96** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

38. *Mheshimiwa Spika*, Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2019 hadi Machi, 2020 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma pamoja na Taasisi zake ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

- (i) Uandaaji wa Nyaraka za kisera katika Wizara 15 ulifanyiwa uchambuzi ili kuondoa migongano na urudufu wakati wa utekelezaji na kuimarisha uzingatiaji wa mipaka ya utekelezaji;
- (ii) Kanuni za Utumishi wa Umma zimefanyiwa mapitio ili kukidhi mahitaji ya sasa ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Kanuni hizo zitaanza kutumika baada ya kuidhinishwa;
- (iii) Miundo ya Maendeleo ya Utumishi ya taasisi 54 ilihuishwa ili kuwianisha na kuoanisha mishahara katika Utumishi wa Umma kwa kuzingatia matokeo ya zoezi la Tathmini ya Kazi. Kati ya miundo ya taasisi hizo, miundo ya taasisi 22 iliidhinishwa na Miundo ya taasisi 18 tayari imeanza kutekelezwa;
- (iv) Taasisi za Umma 26 zilifanyiwa ufuatiliaji ambao umebaini kuongezeka kwa utekelezaji bora wa afua za UKIMWI. Vile vile, taasisi hizo zilihamasishwa kuhusu ujumuishwaji zaidi wa masuala ya Anuai za Jamii (Jinsia, UKIMWI na Ulemavu) katika Utumishi wa Umma ili kutoa huduma jumuishi kwa wananchi;

- (v) Nyaraka nne za Kiutumishi zilitolewa ili kuimarisha Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Nyaraka hizo ni Waraka wa Matumizi ya magari ya Serikali; Waraka wa Utumishi kuhusu ufanuzi wa utaratibu wa Mawasiliano Serikalini; Waraka wa Utumishi kuhusu Utaratibu wa Kutekeleza Maelekezo/Maagizo yanayotolewa na Viongozi kwa njia ya mdomo; Waraka wa Watumishi wa Umma kuhusu Utaratibu wa Kukopesha Fedha Taslimu Watumishi wa Umma kwa ajili ya Kununulia Magari/Pikipiki, Samani au Matengenezo ya Magari/Pikipiki;
- (vi) Nyumba 477 kwa ajili ya watumishi wa umma, sekta binafsi na wanachama wa mifuko ya hifadhi ya jamii zilijengwa kupitia Watumishi Housing katika maeneo ya Dodoma (100), Dar es Salaam (268), Morogoro (50) na Mwanza (59) na kuziwa kwa masharti nafuu.
- (vii) Uwekaji wa miundombinu ya barabara, umeme na maji kwenye nyumba 68 zilizojengwa Dar-es-salaam na Watumishi Housing umefanyika;
- (viii) Miundo na Mgawanyo wa Majukumu 114 ilihuishwa na kuidhinishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, miundo hiyo ni ya Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali na Mashirika ya Umma;
- (ix) Taasisi za Umma sita zimewezeshwa kuandaa Maelezo na Orodha ya Kazi kwa Taasisi;

- (x) Uainishaji wa aina ya mafunzo ya ufuatiliaji na tathmini yanayohitajika kwa watumishi wa Umma kwa kila ngazi ya Serikali umeratibiwa na kutambua mahitaji kwa kushirikisha wadau wa Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini;
- (xi) Vikao viwili vya Wadau wa Ufuatiliaji na Tathmini viliratibiwa na kufanyika ili kupata maoni ya namna bora ya kuunda na kutekeleza Mifumo ya Ufuatiliaji na Tathmini Serikalini;
- (xii) Miongozo ya viwango mbalimbali vya kuboresha utendaji kazi serikalini imeandaliwa na kusambazwa katika taasisi za Umma. Miongozo hiyo ni pamoja na Mwongozo wa Uandishi wa Nyaraka mbalimbali za Serikali; Mwongozo wa Karatasi Maalum ya Barua yenye Anwani (Letter Heads) na Mwongozo wa Kitambulisho cha Mtumishi wa Umma;
- (xiii) Mifumo ya Utendaji Kazi katika taasisi za Umma imehuishwa ambayo ni Mpango Mkakati wa Taasisi (Taasisi sita); Mkataba wa Huduma kwa Mteja (Taasisi sita) na Nyenzo ya kufanya Tafiti ya Utoaji Huduma (Taasisi moja);
- (xiv) Watumishi wa Umma 290,625 wa Kada mbalimbali walipandishwa vyeo. Aidha, Vibali vya ajira mpya na mbadala katika utumishi wa umma vyenye nafasi 6,975 kwa kada mbalimbali vimetolewa ili kuimarisha utendaji katika utumishi wa umma;

- (xv) Taasisi za Umma zote zimewezeshwa kuandaa makadirio ya mishahara ya watumishi wake kwa kutumia Mwongozo wa Ikama na Bajeti ya Mishahara ya watumishi wa Umma kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021;
- (xvi) Madai ya malimbikizo ya mishahara kwa watumishi wa Umma **14,761** yenyeye thamani ya **Shilingi 33,326,487,212.05** yalilipwa, hivyo kufanya idadi ya watumishi waliolipwa madai yao tangu Serikali ya Awamu ya Tano iingie madarakani kufikia **100,684** ambao walilipwa kiasi cha **Shilingi 130,426,656,606.14**. Vile vile, madai ya watumishi **13,058** yenyeye thamani ya **Shilingi 33,715,291,606.05** yamehakikiwa na kuwasilishwa Hazina kwa uhakiki na malipo. Aidha, madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi wa umma **23,923** yenyeye thamani ya **Shilingi 54,673,930,534.96** yanaendelea kuhakikiwa na OR-MUU;
- (xvii) Ukaguzi wa Matumizi na usimamizi sahihi wa Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS) umefanyika katika Wizara, Idara Zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi za Umma;

- (xviii) Usafishaji (uwekaji wa taarifa za kila mtumishi kwa usahihi) na Uboreshaji waTaarifa za Kiutumishi na Mishahara za watumishi kwa waajiri wote wanaotumia Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS) umefanyika;
- (xix) Utoaji huduma kwa waajiri mbalimbali uliwezeshwa kwa kutoa vibali vya uhamisho vya watumishi wa umma 4,144, kuazimwa 650, kushikizwa 26 na likizo bila malipo 180;
- (xx) Katika kuwezesha waajiri kujaza nafasi za uongozi kwenye taasisi zao, mapendelekezo ya nafasi za uteuzi 1,374 yalipokelewa, kati ya hayo 1,183 sawa na asilimia 86 yalirejeshwa kwa waajiri kwa utekelezaji. Aidha, vibali vya uteuzi 116 vimetolewa kwa nafasi za uongozi ambazo zilipendekezwa kwa afisa zaidi ya mmoja, mikataba ya ajira 94 imeshughulikiwa na vibali 263 vya kukaimu nafasi za uongozi vimetolewa;
- (xxi) Watumishi wa Umma 885 walijengewa uwezo kwa kupewa nafasi za mafunzo nje ya nchi katika fani mbalimbali zikiwemo Kilimo, Madini, Afya, Nishati, Elimu na TEHAMA. Fursa hizo za mafunzo zilitolewa kwa Ufadhilli wa Serikali na Wadau wa Maendeleo ambao ni Serikali ya Jamhuri ya Korea (64); Serikali ya India (229); Serikali ya Japan (85); Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China (465); na Serikali ya Australia (42);

- (xxii) Viongozi 16 wa Serikali waliwezeshwa kubadilishana uzoefu wa utendaji kazi mionganini mwa nchi zao. Viongozi 10 wa Serikali walihudhuria Mkutano wa 4 wa Jumuiya ya Utawala wa Utumishi wa Umma na Usimamizi Barani Afrika uliofanyika Cairo-Misri. Vile vile, Viongozi sita walihudhuria Mkutano wa sita wa Mtandao wa Mameneja wa Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma uliofanyika Rabbat – Morocco;
- (xxiii) Mamlaka ya Udhibiti wa Bima Tanzania na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania zimevezeshwa kuandaa Mipango ya Rasilimaliwatu itakayozivezesha taasisi hizo kufikia malengo ya mipango mkakati iliyojiveke;
- (xxiv) Taasisi za Umma Sita zimevezeshwa kuandaa Mipango ya Urithishanaji Madaraka ili kuwaandaa na kuwajengea uwezo watumishi waweze kumudu majukumu ya nafasi za uongozi na kufanya taasisi ziendelee kutoa huduma bora. Taasisi hizo ni Mamlaka ya Vitambulishio vya Taifa; Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania; Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania; Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya; Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam; na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki;
- (xxv) Taasisi saba zilijengewa uwezo wa namna ya kufanya Tathmini ya Mahitaji ya Mafunzo na

kuandaa mipango ya mafunzo. Taasisi hizo ni Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga; Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania; Chuo cha Teknolojia Dar es Salaam; Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania; Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania; Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya; na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa;

(xxvi) Ufutiliaji wa uzingatiaji wa Maadili ulifanyika kwenye taasisi za Umma 29 kati ya 31 zilizokusudiwa. Aidha, matokeo ya Ufutiliaji wa Uzingatiaji wa Maadili katika taasisi 13 kwa mwaka 2018/19 yalionesha kiwango cha uzingatiaji wa Maadili kilifikia asilimia 79 ikiwa ni ongezeko la asilimia 4 kutoka tathmini ya mwaka uliotangulia;

(xxvii) Ufutiliaji wa ushughulikiaji wa malalamiko ya wananchi katika taasisi za Umma umeonesha kiwango cha ushughulikiaji kimefikia asilimia 84 ambapo jumla ya malalamiko 588 yalishughulikiwa kati ya 698 yaliyopokelewa. Kiwango hiki ni ongezeko la asilimia 26.7 ikilinganishwa na mwaka uliotangulia;

(xxviii) Kampeni za ukuzaji maadili katika menejimenti za taasisi za Umma zilifanyika kupitia mafunzo ya maadili ya utendaji kwa menejimenti na watumishi 266 kutoka Sekretarieti ya Mkoa wa Katavi na Ofisi za Wakuu wa Wilaya tano na Mamlaka za Serikali za Mitaa sita;

- (xxix) Uhamasishaji wa uadilifu katika Utumishi wa Umma ulifanyika katika Wiki ya Uadilifu na kuhitimishwa Kitaifa tarehe 11/12/2019 kwa kushirikiana na taasisi saba zinazosimamia Maadili katika Utumishi wa Umma;
- (xxx) Uhamasishaji wa ukuzaji wa maadili umeendelea kufanyika ambapo watumishi 2,654 kutoka taasisi 22 za Umma wamepatiwa mafunzo ya maadili. Vile vile, vipindi 10 vya redio na vipindi nane vya runinga vinavyohusu Ukuzaji wa Maadili na Uzingatiaji wa Maadili katika Utumishi wa Umma vimeendelea kurushwa katika Redio na Runinga mbalimbali nchini;
- (xxxi) Uimarishaji wa usimamizi wa TEHAMA Serikalini umefanyika kwa kuwezesha utungwaji wa sheria ya Mamlaka ya Serikali Mtandao. Maandalizi ya msingi ya utekelezaji wa Mamlaka hiyo yamekamilika;
- (xxxii) Maandalizi ya uanzishwaji wa vituo vya Huduma Pamoja yamefanyika ambapo Mshauri Mwelekezi wa kutathmini huduma zinazotolewa na Serikali na miundombinu iliyopo kwa ajili hiyo ameanza kazi kwa kutembelea wadau mbalimbali Dodoma, Dar es Salaam na Zanzibar;
- (xxxiii) Ujenzi wa mfumo mpya wa HCMIS kwa kutumia wataalam na fedha za ndani umekamilika na kufanyiwa majaribio ndani ya

taasisi. Mfumo huu una uwezo mkubwa wa kusimamia masuala ya kiutumishi ikilinganishwa na Mfumo unaotumika sasa. Aidha, zoezi la kuhamisha taarifa kutoka mfumo wa sasa kwenda mfumo mpya na mpango wa mafunzo kwa watumiaji wa mfumo mpya unaendelea. Vile vile, mfumo huu utaunganishwa na mifumo mingine kama e-OPRAS, Mahudhurio ya Kielektroniki na Vitambulisho vya Taifa;

(xxxiv) Mafunzo ya namna ya kutumia Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS – Lawson) ili kuwa na uendelevu wa utoaji huduma yametolewa kwa Maafisa Utumishi/Tawala 220 kutoka Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(xxxv) Taasisi za Umma 34 zilijengewa uwezo kuhusu mfumo wa Mikataba ya Utendaji Kazi Serikalini ili kuimarisha utoaji huduma kwa ngazi ya taasisi. Aidha, taasisi za Umma tano ziliwezeshwa kuandaa Mikataba ya Utendaji Kazi kwa Mtumishi mmoja mmoja. Taasisi hizo ni Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TaEC), OR-TAMISEMI, Shirika la Bima la Taifa, TAKUKURU na Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi;

- (xxxvi) Maandalizi ya Mfumo wa Wazi na Mapitio ya Tathmini ya Utendaji Kazi wa Kielektroniki (e-OPRAS) ambao utatumika kupima utendaji kazi wa watumishi wa Umma yamekamilika;
- (xxxvii) Maandalizi ya kustaa fu kwa watumishi wa umma yametolewa ambapo watumishi watano wa Ofisi waliwezeshwa kuhudhuria mafunzo ya wiki moja ya kujiandaa kustaa fu yaliyotolewa na Chuo cha Utumishi wa Umma mkoani Morogoro;
- (xxxviii) Programu ya Maboresho katika Utumishi wa Umma imeandaliwa na kukamilika. Hatua inayoendelea ni kutafuta rasilimalifedha za utekelezaji. Hata hivyo, Ofisi kuitia fedha za ndani imanzisha utekelezaji wa baadhi ya maeneo ya matokeo ya programu hiyo yanayojumuisha ujenzi wa Mifumo ya kielektroniki na kuingizwa katika michakato ya utekelezaji wa utoaji huduma kwa Umma;
- (xxxix) Makala kuhusu mafanikio ya miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Tano katika eneo la Utumishi wa Umma iliandaliwa na kuchapishwa katika jarida maalum la Nchi Yetu Toleo Na. 232 la Novemba, 2019 linalotolewa na Idara ya Habari MAELEZO;
- (xli) Umma umehabarishwa kuhusu ajira zilizotolewa na Serikali kwa wahitimu wa mafunzo ya JKT “Operesheni Magufuli” waliojitolea kwa kipindi cha kuanzia miaka miwili, ambapo wahitimu

1,500 walijitokeza kuomba ajira ili wawe sehemu ya kuimarisha utendaji kazi katika taasisi za Umma; na

- (xli) Huduma kwa Viongozi Wakuu wa Kitaifa (Wastaafu 11 na wajane 5) zimetolewa kwa mujibu wa Sheria.

b. Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC)

39. *Mheshimiwa Spika*, Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania kilianzishwa ili kutoa mafunzo, ushauri, kufanya utafiti tumizi na kutoa machapisho mbalimbali katika nyanja za Uongozi, Menejimenti na Utawala. Aidha, Chuo kinaendesha kozi za kitaaluma kwa ngazi za Cheti, Stashahada na Shahada katika nyanja za Uhazili, Utunzaji Kumbukumbu, Menejimenti ya Rasilimali Watu, Utawala na Ununuzi wa Umma. Chuo kinatekeleza majukumu hayo katika Kampasi sita zilizoko kwenye Mikoa ya Dar es Salaam, Tabora, Mtwara, Singida, Tanga na Mbeya.

40. *Mheshimiwa Spika*, utoaji wa mafunzo kwa watumishi wa Umma umeendelea kuimarisha ili kuwajengea uwezo katika utendaji kazi na kutoa huduma bora kwa wananchi. Katika kuhakikisha kuwa mafunzo yanayotolewa kwa watumishi wa Umma yanaimarisha utendaji kazi wao, Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao (TaGLA) iliunganishwa na Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania kuitia Tangazo la Serikali Na. 63 lilitolewa katika Gazeti la Serikali la

Tarehe 31 Januari, 2020. Hivyo, kwenye Wasilisho la Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/21, majukumu ya TaGLA yataonekana katika majukumu ya Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania.

41. *Mheshimiwa Spika*, Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2019 hadi Machi, 2020 Chuo cha Utumishi wa Umma kimetekeleza shughuli zifuatazo:-

- (i) Watumishi wa Umma 1,014 walipatiwa mafunzo ya kijiandaa kufanya Mitihani ya Utumishi wa Umma ambayo yamelenga kuimarisha uwezo wa utendaji kazi, hiyo ni sawa na asilimia 105 ya Watumishi waliolengwa;
- (ii) Watumishi wa Umma 2,805 wamepatiwa Mafunzo ya Uongozi na Maendeleo pamoja na Menejimenti na Usimamizi wa Ofisi katika Taasisi za umma, hiyo ikiwa ni sawa na asilimia 83 ya lengo la mwaka;
- (iii) Mafunzo ya Awali yalitolewa kwa Watumishi wa Umma wapya 2,116 ili kujenga uelewa wa utendaji kazi wa Serikali;
- (iv) Wanafunzi 10,902 sawa na asilimia 109 walidahiliwa katika ngazi ya Shahada ya Kwanza, Stashahada na Cheti, kwa ajili ya mafunzo ya muda mrefu katika fani za utunzaji wa kumbukumbu, uhazili, TEHAMA, utunzaji wa fedha za umma, na Menejimenti ya

Rasilimaliwatu, Usimamizi wa Ununuzi wa Umma na Uongozi na Utawala Bora;

- (v) Maandiko ya ushauri katika maeneo sita ya kitaalamu yameandaliwa na kuwasilishwa kwa wateja. Aidha, ushauri katika maeneo manne ya kitaalam katika Menejimenti ya Utumishi wa Umma ultolewa;
- (vi) Utafiti katika maeneo mawili yanayolenga kuboresha Utumishi wa Umma umeanzishwa;
- (vii) Makala tano za kitaalamu katika Utumishi wa Umma zimechapishwa katika majarida mbalimbali ndani na nje ya nchi. Aidha, Jarida moja la Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC Journal) lipo katika hatua za uchapishaji;
- (viii) Watumishi 81 wa Chuo cha Utumishi wa Umma wamejengewa uwezo katika taaluma mbalimbali, kama ifuatavyo: Shahada ya Uzamivu (sita), Shahada ya uzamili (watatu) na mafunzo ya muda mfupi watumishi (72);
- (ix) Ujenzi wa awamu ya pili wa jengo la madarasa, maktaba na ofisi katika Kampasi ya Tabora lenye ghorofa mbili umekamilika. Aidha, ukarabati wa paa za njia kwenda kwenye madarasa na Hostel iitwayo Oysterbay umekamilika;
- (x) Uandaaji wa michoro ya usanifu majengo kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa majengo ya Kampasi ya Dodoma umeanzishwa; na

- (xi) Eneo kwa ajili ya ujenzi wa Kampasi ya Tanga limepatikana na mchakato wa umilikishwaji umeanzishwa.

c. Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao (TaGLA)

42. *Mheshimiwa Spika*, Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao (TaGLA) ina jukumu la kuwajengea uwezo Watumishi wa Umma na Sekta binafsi kwenye maeneo mbalimbali kwa kuratibu na kuendesha mafunzo na midahalo maalum ya muda mfupi kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ili kuhimili kasi ya mabadiliko ya utoaji wa huduma kwa wananchi.

43. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2019 hadi Machi, 2020 Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao imetekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Huduma za maunganisho ya kuwezesha mafunzo kwa njia ya mtandao kwa washiriki 1,640 kutoka Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali na sekta binafsi zimetolewa. Mafunzo haya yalitolewa katika maeneo ya Uongozi na Menejimenti, Utawala Bora, Maadili, Anuai za Jamii, Mazingira, TEHEMA, Afya na Stadi za utendaji kazi;
- (ii) Mafunzo yametolewa kwa washiriki 516 kwa kwa njia ya video ndani na nje ya nchi. Midahalo hiyo ilijumuisha kubadilishana uzoefu wa Mfumo wa Upimaji wa Wafanyakazi na Usimamizi wa Bajeti

kutoka Serikali ya Korea kwa kushirikiana na Chuo cha Maendeleo cha Korea Kusini (KDI). Pia midahalo 24 ya ndani na nje ya nchi imeratibiwa na kufanyika. Midahalo hii ni pamoja na Majiji Endelevu, Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza, Midahalo ya Jumuiya ya Wanasheria Tanganyika (TLS), matumizi ya TEHAMA serikalini na midahalo ya Afya na Mazingira;

- (iii) Matumizi ya vifaa vyta mawasiliano kwa njia ya video na mfumo wa mawasiliano ndani na nje ya nchi vyta Wakala yamesimamiwa na kufanyiwa matengenezo;
- (iv) Elimu kwa wadau ilitolewa juu ya manufaa ya kutumia Teknolojia ya Mawasiliano na Habari (TEHAMA) kwa njia ya mtandao wa video. Wadau hao ni Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, NIMRI, African Legal Support Facility (ALSF), DAWASA, Wizara ya Mawasiliano ya Lesotho, Tume ya Utumishi wa Umma ya Zimbabwe, Shirika la Posta Tanzania na Jumuia ya Wanasheria Tanganyika;
- (v) Wigo wa huduma za Wakala uliongezwa kwa wateja 287 katika Kituo cha Wakala cha Morogoro. Aidha, Wakala imewajengea uwezo watumishi wake ili kuimarisha utendaji wa kazi. Watumishi sita walipata mafunzo ya muda mfupi, kati yao hao watumishi wanne wamepata mafunzo ya ndani ya nchi na watumishi wawili wamepata mafunzo nje ya nchi. Aidha, mtumishi mmoja amemaliza

mafunzo ya Shahada ya Uzamili katika fani ya Usimamizi wa Rasilimaliwatu kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe; na

(vi) Elimu juu ya jinsi ya kuratibu mikutano, midahalo na mafunzo ilitolewa. Aidha, Ushauri ultolewa juu ya Ufungaji Bora wa Vifaa, sifa zake, mazingira ya chumba kwa ajili ya mikutano au mafunzo na mitambo stahiki ya mawasiliano kwa njia mtandao wa video. Vile vile, ushauri wa kitaalamu na kubadilishana uzoefu ultolewa kwa taasisi nne za Serikali zikiwepo Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali (MDA).

d. Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA)

44. *Mheshimiwa Spika*, Wakala ya Serikali Mtandao imebadilika na kuwa Mamlaka ya Serikali Mtandao kwa mujibu Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya Mwaka 2019 ambayo imeanza rasmi tarehe 15/12/2019 kwa Tangazo la Serikali Na. 964 la tarehe 6/12/2019. Sheria hii inaipa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) majukumu na nguvu ya kuratibu, kusimamia na kukuza jitihada za serikali mtandao.

45. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi hiki cha Awamu ya Tano, Mamlaka ya Serikali Mtandao, kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango, imeimarisha na kujenga mifumo imara ya kusimamia ukusanyaji wa mapato katika Taasisi za Serikali zikiwemo Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mifumo hiyo

imesaidia sana kurahisisha ukusanyaji wa mapato, kuziba mianya ya upotevu wa fedha za umma na kuwezesha ongezeko la ukusanyaji wa mapato katika sekta mbalimbali za Serikali kuanzia Serikali Kuu hadi Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hadi sasa Taasisi za Umma 631 na watoa huduma za malipo 19 zikiwemo Benki na Kampuni za Simu zimeunganishwa katika Mfumo Mkuu wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato Serikalini “Government e-Payment Gateway – GePG”.

46. *Mheshimiwa Spika*, Mamlaka pia imejenga uwezo wa wataalam wa TEHAMA serikalini na kuwezesha mifumo ya TEHAMA ya Serikali kujengwa kwa kutumia wataalam wa ndani tofauti na awali ambapo mifumo hiyo ilikuwa inanunuliwa. Hatua hii imesaidia kuokoa gharama za ubunifu, ujenzi na uendeshaji wa mifumo hiyo pamoja na kuimarisha usalama wa mifumo husika.

47. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Mamlaka imetekeleza shughuli zifuatazo:-

- (i) Mamlaka imeunganisha taasisi za Umma zilizopo Dodoma kwenye Mtandao wa Mawasiliano Serikalini ili kuwezesha mawasiliano mionganini mwa taasisi za Serikali, pamoja na kuongeza na kuboresha usalama wa taarifa na kupunguza gharama za mawasiliano. Aidha, Mamlaka imekamilisha ukarabati wa Kituo cha Utafiti,

Ubunifu na Maendeleo ya Serikali Mtandao katika eneo la Chuo Kikuu cha Dodoma, ambapo wanafunzi 33 kutoka UDOM, UDSM, NM-Aist, DIT, Chuo Kikuu cha St.Joseph, na MUCE wameshiriki katika kazi mbali mbali za utafiti na ubunifu;

- (ii) Uboreshaji wa utoaji wa huduma kwa wananchi umefanyika kwa kuandaa na kusimamia uendeshaji wa Mifumo na Miundombinu Shirikishi ya TEHAMA ikiwemo; Mtandao wa Mawasiliano Serikalini (Govnet), ambapo taasisi mpya 27 zimeunganishwa hivyo kufanya jumla ya taasisi zilizouanganishwa kufikia 245; Mfumo wa Kutoa Huduma kwa Njia ya Simu za Mkononi ambapo taasisi mpya 13 zimeunganishwa na hivyo kufanya jumla ya taasisi zilizouanganishwa kufikia 160; Mfumo wa Ofisi Mtandao ambapo taasisi mpya 18 zimeunganishwa na kufanya jumla ya taasisi zote kufikia 77; Mfumo wa Mawasiliano kwa Njia ya Barua Pepe ambapo taasisi mpya 30 zimeunganishwa na kufanya jumla ya taasisi zote kufikia 426;
- (iii) Taasisi mpya 26 zimeunganishwa na kutumia huduma ya vituo vya kisasa na mahsus (Data Centres) kwa ajili kuhifadhi Mifumo ya Serikali Mtandao na taarifa ili kuboresha mazingira, kuongeza usalama na kupunguza gharama ya kuhifadhi rasilimali shirikishi miongoni mwa taasisi za umma na kufanya jumla ya taasisi zinazotumia

huduma hiyo kufikia 75. Aidha, Mamlaka imeanza ujenzi wa Mfumo Maalum utakaowezesha Mifumo mbalimbali ya TEHAMA Serikalini kubadilishana tarifa;

- (iv) Usimamizi wa shughuli za taasisi umeboreshwa kwa kutengeneza Mfumo Shirikishi wa Kusimamia Shughuli na Rasilimali za Taasisi. Mfumo huo unafanya kazi kupitia moduli zinazowasiliiana na kuunganisha shughuli za Idara na Vitengo kielektroniki. Hadi sasa mfumo huu unatumiwa na taasisi 19;
- (v) Mamlaka imeshirikiana na taasisi za umma katika kubuni na kutengeneza mifumo mbalimbali kama vile; Mfumo wa Kukusanya Ushuru wa Magari Daraja la Kigamboni; Mfumo wa Tiketi wa Kielektroniki wa Kampuni ya Huduma za Meli; Mfumo wa Kielektroniki wa Dirisha Moja; Mfumo wa Usimamizi wa Miradi ya TEHAMA Serikalini; Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili unaotumiwa na Baraza la Kiswahili; Mfumo Maalum wa Kusimamia Mafunzo na Semina; Mfumo wa Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Mahesabu; Mfumo wa Bodi ya Wahandisi; Mfumo wa Bodi ya Wataalamu wa Ununuvi; Mfumo wa kuingiza taarifa na nyaraka kwa Sekta ya Afya; Mfumo wa Usimamizi wa Rasilimaliwatu Serikalini; Mfumo wa Sekta ya Maji utakaotumika na Mamlaka zote za Maji nchini; Mfumo wa Idara ya Wakili Mkuu wa

Serikali; Mfumo wa Kuhifadhi Taarifa za Vifaa vya Maktaba ya Bunge na Mfumo wa Bunge Mtandao. Ubunifu huu, umesaidia Serikali ya awamu ya Tano kuokoa fedha nyingi ambazo zingetumika, iwapo mifumo hiyo ingejengwa na wakandarasi;

- (vi) Mafunzo kwa taasisi 92 yametolewa katika maeneo ya usimamizi wa Mtandao wa Mawasiliano Serikalini ikiwemo, Mfumo wa Barua Pepe; Mfumo wa Ofisi Mtandao; Mfumo wa Vibali vya Kusafiri Nje ya Nchi; Mfumo wa Kusimamia Rasilimali za Taasisi; Utoaji wa huduma mtandao kwa umma; na usimamizi wa tovuti;
- (vii) Huduma za ushauri kuhusu uhakiki wa Mifumo ya TEHAMA, Tathmini ya Usalama, Utayarishaji wa Mpango wa Kukabili Majanga, Utayarishaji wa Sera na Mikakati ya TEHAMA ya taasisi, Usanifu wa Shughuli na Tathmini ya Miradi ya TEHAMA zimetolewa kwa taasisi 35 ili kuhakikisha uwekezaji unaofanywa na Serikali kwenye TEHAMA unaleta matokeo yaliyokusudiwa;
- (viii) Msaada wa kiufundi na ushauri umetolewa kwenye taasisi za umma kupitia Dawati la Msaada wa Huduma kwa Wateja;
- (ix) Usimamizi wa viwango na miongozo ya matumizi ya TEHAMA Serikalini umefanyika ili kuondoa urudufu, kupunguza gharama, kuongeza ubora wa huduma zinazotolewa kwa umma na kuhakikisha usalama wa mawasiliano;

- (x) Watumishi 73 wamewezeshwa kuhudhuria mafunzo ya kitaalam ya muda mfupi na muda mrefu yanayoendeshwa na Bodi mbali mbali za kitaaluma; na
- (xi) Ujenzi wa kituo cha usaidizi wa masuala ya Serikali Mtandao kwenye Mji wa Serikali Mtumba - Dodoma umekamilika na uwekaji wa vifaa vitakavyoimarisha mawasiliano katika mji huo unaendelea.

OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA

48. *Mheshimiwa Spika*, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma (imeanzishwa kwa mujibu wa Kifungu 29 (1) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298.

49. *Mheshimiwa Spika*, Katika Mwaka wa Fedha 2019/20 Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma iliidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 2,376,443,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Machi, 2020, kiasi cha **Shilingi 1,676,457,590** za Matumizi ya Kawaida zilitolewa na kutumika.

50. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Sekretarieti imetekeleza shughuli zifuatazo:-

- (i) Matangazo 51 ya nafasi za ajira yaliandaliwa na kutolewa kwa niaba ya waajiri 83 katika Utumishi wa Umma ambao ni Wizara tano, Idara Zinazojitegemea sita, Mashirika ya Umma 12, Wakala za Serikali sita, Mamlaka sita, Taasisi 25 na Vyuo vya Elimu ya Juu 23;
- (ii) Usimamizi na uendeshaji wa michakato ya ajira umefanyika mara sita kwa niaba ya waajiri 83 ambapo wasaililiwa 2,968 waliofaulu usaili walipangwa katika vituo vya kazi vifuatavyo: Mamlaka za Serikali (932), Mashirika ya Umma (1,097), Wakala za Serikali (235), Wizara (158), Mamlaka za Serikali za Mitaa (271), Taasisi za Elimu (175), Idara Zinazojitegemea (watano) na Sekretarieti za Mikoa (95). Aidha, kati ya waajiriwa hao 17 ni wenyе mahitaji maalum, kati ya hao wanawake ni saba na wanaume ni kumi;
- (iii) Utaalam wa masuala ya uendeshaji wa mchakato wa ajira ultolewa kwenye usaili uliofanyika mara 14 kwenye taasisi zilizokasimiwa kuendesha usaili kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 922 la Tarehe 29 Novemba, 2019. Mamlaka zilizohusika ni Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga, Halmashauri za Wilaya za Biharamulo (usaili mara mbili), Bukoba, Kondoa, Dodoma, Busega, Kaliua,

Tanga Muheza, Meru na Mbulu, Bagamoyo na Illeje. Taarifa za usaili ulifanyika zimeandaliwa na kuhifadhiwa kwa ajili ya kumbukumbu na rejea. Aidha, usaidizi wa utaalam ultolewa kwenye usaili wa taasisi za elimu ya juu ulifanyika mara sita. Taasisi hizo ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu Mzumbe, Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania, Chuo cha Uhasibu Tanzania, Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine na Chuo Kikuu Kishiriki Cha Elimu Mkwawa;

- (iv) Usimamizi na uendeshaji wa mchakato wa kumpata mwakilishi wa kanda ya Afrika kugombea nafasi ya Katibu wa Bunge la Jumuiya ya Madola ulifanyika kwa kushirikiana na Ofisi ya Bunge la Tanzania;
- (v) Mfumo wa maombi ya kazi kwa njia ya kielektroniki ‘Recruitment Portal’ umekamilika. Mfumo huo umeunganishwa na mifumo ya Serikali ikiwemo ya NIDA, NECTA, NACTE na OR-MUUUB;
- (vi) Mfumo wa Mawasiliano ya Ndani (intranet) umekamilika na kuanza kutumika. Mfumo huu umeboresha mawasiliano ndani ya Sekretarieti ya Ajira;
- (vii) Ukaguzi wa vyeti 8,079 vya waombaji ulifanyika ili kuhakiki usahihi wa taarifa za waombaji kazi ambapo vyeti 58 viligundulika kuwa ni vya kugushi;
- (viii) Usimamizi wa mitihani ya mchujo na ya vitendo kwa kada mbalimbali ulifanyika;

- (ix) Huduma za kiutawala na kiutumishi kwa Ofisi ya Zanzibar zilitolewa;
- (x) Usambazaji wa Kanuni za Uendeshaji za Sekretarieti ya Ajira kwa Halmashauri za Tanzania Bara umefanyika;
- (xi) Utatuzi wa changamoto za kada ya udereva zilijadiliwa baina ya Sekretarieti na wadau wa usafirishaji ambao ni Chuo Cha Taifa cha Usafirishaji, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis na Chama cha Wamiliki wa Shule Binafsi za Udereva; na
- (xii) Elimu kwa Umma kuhusu shughuli za Sekretarieti ya Ajira ilitolewa kuitia Makala na vipeperushi mbalimbali pamoja na mikutano sita ya vyombo vya habari. Aidha, taarifa za maboresho ya mifumo ya ajira zimekuwa zikiuhishwa katika tovuti ya taasisi na mitandao ya kijamii.

OFISI YA RAIS, TUME YA UTUMISHI WA UMMA

51. *Mheshimiwa Spika*, Tume ni chombo rekebu na inayo mamlaka na wajibu wa kuhakikisha kuwa masuala ya Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma yanasihamiwa na kuendeshwa kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu mbalimbali kama inavyotolewa na Mamlaka. Wajibu huu wa Tume una lengo la kuimarisha Utawala Bora unaozingatia matokeo. Katika kutekeleza wajibu huu pamoja mambo mengine Tume imeendelea kufanya ukaguzi wa

Rasilimaliwatu kwa Mamlaka za Ajira na Nidhamu. Aidha, Tume ya Utumishi wa Umma ni Mamlaka ya Rufaa kwa Watumishi wa Umma dhidi ya Uamuzi unaotolewa na mamlaka zao za nidhamu.

52. *Mheshimiwa Spika*, Katika Mwaka wa Fedha 2019/20 Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma iliidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 4,889,515,606** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Machi, 2020 kiasi cha **Shilingi 3,279,257,786.98** za Matumizi ya Kawaida zilitolewa na kutumika.

53. *Mheshimiwa Spika*, Katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi, 2020 Tume imetekeleza majukumu yafuatayo:-

- (i) Uzingatiaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu katika usimamizi wa Utumishi wa Umma umesimamiwa kwa kufanya ukaguzi katika taasisi 77;
- (ii) Maamuzi ya rufaa 138 yalifanyika na malalamiko 504 yalishughulikiwa kupitia mikutano mitatu ya Tume iliyofanyika ;
- (iii) Elimu kwa wadau kuhusu majukumu ya Tume na Utekelezaji wa Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Utumishi wa Umma ilitolewa kwa taasisi za umma 21. Aidha, kupitia ziara ya Makamishna wa Tume, elimu ilitolewa kuhusu Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298 na haki na

wajibu wao kwa watumishi wa umma 1,070 wakiwemo Viongozi wa Taasisi za Umma ambao ni Wakuu wa Mikoa (Mwanza na Simiyu), Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri, Makatibu Tawala wa Wilaya, Watendaji Wakuu wa Wakala za Serikali, Taasisi za Umma na Watumishi wa Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri. Vile vile, elimu ilitolewa kuitia kurusha vipindi sita hewani vya Runinga na vipindi sita vya Redio. Pia, kuitia maadhimisho ya Wiki ya Maadili na Haki za Binadamu wadau wa Tume walipatiwa elimu kuhusu Sheria Na. 8 na Kanuni zake;

- (iv) Taarifa ya Hali ya Utumishi wa Umma na Utekelezaji wa Majukumu ya Tume ya Mwaka 2018/19 iliandaliwa na kuwasilishwa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
- (v) Utekelezaji wa mahitaji ya anuai za jamii katika utumishi wa umma ulifanyika kwa kuwapatia huduma watumishi wa Tume wenye uhitaji maalum kulingana na Miongozo iliyopo; na
- (vi) Watumishi 209 wa Tume wamewezeshwa kupata mafunzo ambapo watumishi 17 walihuduria mafunzo ya muda mrefu, watumishi 100 walihuduria mafunzo ya muda mfupi katika maeneo ya uadilifu na OPRAS. Vile vile, watumishi 92 walipatiwa mafunzo maalum ya

Uchambuzi wa Rufaa na Uguzi wa Rasilimali Watu.

BODI YA MISHAHARA NA MASILAHI KATIKA UTUMISHI WA UMMA

54. *Mheshimiwa Spika*, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma ina jukumu la kufanya mapitio ya mara kwa mara na kupendekeza viwango vya mishahara na masilahi mengine; na kuzishauri mamlaka kuhusu misingi ya miundo ya mishahara katika Utumishi wa Umma.

55. *Mheshimiwa Spika*, Katika Mwaka wa fedha 2019/20, Bodi iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,474,241,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020, **Shilingi 1,040,580,328** zilipokelewa na kutumia.

56. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi, 2020, Bodi imetekeleza majukumu yafuatayo:-

- (i) Maandalizi kwa ajili ya ushauri kuhusu masilahi kwa watumishi wa Umma yamefanyika kwa kufanya utafiti wa mapitio ya Mipango ya Motisha katika Serikali Kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kukusanya taarifa kutoka taasisi 94 za Umma na uchambuzi wa taarifa hiyo unaendelea;

- (ii) Mapitio ya mwenendo wa bajeti ya mishahara ya watumishi wa umma kwa kipindi cha miaka 10 yamefanyika. Aidha, rasimu ya taarifa hiyo imeandaliwa na kujadiliwa na wadau kabla ya kuiwasilisha Serikalini; na
- (iii) Taarifa kuhusu gharama za maisha kama msingi wa kukadiria kiwango cha mshahara wenyе staha kwa watumishi wa Umma imeandaliwa na kuwasilishwa kwenye mamlaka husika; na
- (iv) Mkutano wa wadau kuhusu uboreshaji wa utendaji kazi na kuongeza tija katika utumishi wa Umma ulifanyika. Maoni yaliyotolewa yalichambuliwa na mapendekezo yamewasilishwa serikalini.

OFISI YA RAIS, IDARA YA KUMBUKUMBU NA NYARAKA ZA TAIFA

57. *Mheshimiwa Spika*, kwa mujibu wa Sheria ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa Na. 3 ya mwaka 2002, Idara ya Kumbukumbu ya Nyaraka za Taifa imepewa jukumu la kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu za utunzaji kumbukumbu na nyaraka katika Taasisi za Umma. Aidha, Idara ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Kuwaenzi Waasisi wa Taifa Na. 18 ya Mwaka 2004 katika kukusanya, kutunza na kuhifadhi kumbukumbu na vitu vya Waasisi wa Taifa letu (Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume).

58. *Mheshimiwa Spika*, Katika mwaka wa fedha 2019/20, Fungu 4: Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa, iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 4,774,066,000**, kati ya fedha hizo **Shilingi 2,774,066,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 2,000,000,000** kwa Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2020, **Shilingi 1,836,345,500** za Matumizi ya Kawaida zilipokelewa na kutumika.

59. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 Idara ya Kumbukumbu ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

- (i) Nyaraka za kihistoria zimeendelea kuchambuliwa na kukusanywa kwa lengo la kutunza historia ya nchi yetu. Idara imekusanya nyaraka na machapisho 728 kutoka Taasisi za Umma nne na kuhifadhiwa katika Kituo cha Taifa cha kumbukumbu Dodoma. Taasisi hizo ni Halmashauri ya Jiji la Arusha (161), Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa wa Dar es Salaam (117) na Ofisi za Wakuu wa Wilaya ya Lushoto (365) na Korogwe (85);
- (ii) Ukarabati wa nyaraka zilizohifadhiwa katika Ghala Kuu la Nyaraka umefanyika ambapo nyaraka kongwe 197 zimefanyiwa ukarabati ikiwemo nyaraka zinazomhusu Baba wa Taifa Mwl. Julius K. Nyerere 109, Hansards 32, Ripoti za ukaguzi 22, Mikataba 32 na Act Supplement mbili;

- (iii) Uhifadhi wa kumbukumbu na nyaraka katika mifumo ya kidijitali ili kuweza kudumu muda mrefu, kurahisisha upatikanaji na kulinda nakala halisi umefanyika ambapo majalada 490 yameingizwa kwenye mfumo huo;
- (iv) Mifumo bora ya Utunzaji Kumbukumbu za Kiutendaji imewekwa katika Wizara na taasisi za Umma 25. Aidha, Mfumo wa Kielektroniki wa Masijala umewekwa katika taasisi za Umma saba kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao. Taasisi hizo ni Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Msajili wa Hazina, Wakala wa Vipimo, Bodi ya Manunuzi na Ugavi na Shirika la Reli Tanzania, Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) na Wakala wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi (OSHA);
- (v) Mafunzo ya utunzaji wa kumbukumbu yametolewa katika taasisi za Umma 17 ambazo ni Ofisi ya Rais, Ikulu, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Shirika la Bima la Taifa, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundu, Wakala wa Barabara Tanzania, Tume ya Vyuo Vikuu, Tume ya Taifa ya UNESCO, Shirika la Umeme Tanzania, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Ofisi za Wilaya ya Kisarawe, Chalinze, Kibaha, Mtwara, Mbanga na Moshi na Ofisi za Halmashauri ya Manispaa ya Singida na Iringa;

- (vi) Kumbukumbu tuli za taasisi za Umma tatu ambazo ni Baraza la Mitihani la Taifa, Tume ya Utumishi wa Umma na Chuo cha Uhasibu Tawi la Dar es Salaam zimechambuliwa na kubaini zile zinazostahili kuhifadhiwa na zile ambazo zinastahili kuteketezwa kwa mujibu wa Sheria na Taratibu;
- (vii) Kumbukumbu za Ubalozi wa Tanzania Nchini Kenya zimechambuliwa na kuhamishwa kutoka Nairobi kwenda Kituo cha Taifa cha Kumbukumbu Dodoma ambapo jumla ya majalada 1,059 yenye umuhimu wa kudumu yamehamishwa. Aidha, Majalada yaliyofungwa 21,985 ya mashauri ya Mahakama Kuu Kanda ya Mwanza yakiwemo majalada ya madai 12,128 na jinai 9,857 yalihamishiwa katika Kituo cha Kumbukumbu cha Kanda ya Ziwa Mwanza;
- (viii) Huduma ya utaalam wa kuandaa miongozo ya kutunza na kuteketeza kumbukumbu imetolewa katika taasisi za umma mbili ambazo ni Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi. Aidha, huduma hiyo inaendelea katika Shirika la Viwango Tanzania;
- (ix) Kumbukumbu na nyaraka 3,318 za Waasisi wa Taifa zimechambuliwa na kukusanywa kutoka katika maeneo mbalimbali nchini wakiwemo watu binafsi waliofanya kazi kwa karibu na Waasisi wa

Taifa kwa lengo la kuhifadhi historia ya Nchi yetu;

- (x) Elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kutunza kumbukumbu na nyaraka imetolewa kupitia njia mbalimbali ikiwemo kipindi cha televisheni ya Taifa (TBC) na mitandao ya kijamii. Aidha, Jumla ya wanafunzi 74 kutoka katika Taasisi za Elimu ya Juu walipatiwa mafunzo kuhusu shughuli zinazotekelizwa na Idara. Vyo hivyo ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wanafunzi wanne, Chuo Kikuu Mzumbe wanafunzi 62, Chuo cha Ukutubi Bagamoyo wanafunzi watatu na Chuo cha Kumbukumbu ya Mwl. Nyerere wanafunzi watano;
- (xi) Uwezo wa watumishi umeimarishwa kwa kuwawezesha waajiriwa wapya saba kupata mafunzo ya awali. Aidha, mtumishi mmoja amewezeshwa kuhudhuria Shahada ya Uzamili. Vile vile, mafunzo ya UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza yametolewa kwa watumishi wote wa Idara;
- (xii) Uwezo wa Idara katika ukusanyaji na utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka katika ofisi za Kanda umeongezwa kwa kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Kumbukumbu cha Kanda ya Ziwa-Mwanza; na

(xiii) Ukarabati wa jengo la Idara lililopo Dar es Salaam umekamilika. Aidha, ukarabati wa Ghala la Taifa la kuhifadhi nyaraka unaendelea.

B. MPANGO WA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2020/21 NA MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIWA

60. *Mheshimiwa Spika*, Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/21 umezingatia, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21); Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala ya mwaka 2015; Maelekezo ya Serikali yaliyoainishwa na Mheshimiwa Rais wakati wa uzinduzi rasmi wa Bunge la 11 Mwezi Novemba, 2015; Sheria ya Bajeti, Sura 439 pamoja na kanuni zake; na Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya III.

61. *Mheshimiwa Spika*, Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/21 imezingatia utatuzi wa changamoto katika utoaji huduma kwa umma kwa kadri inavyowezekana. Kwa ujumla changamoto hizo ni kama ifuatavyo: Baadhi ya ofisi za utoaji huduma kutokuwepo katika mikoa yote ya Tanzania; Bado kumekuwepo na malalamiko kutoka kwa wananchi kuhusu upatikanaji wa huduma zitolewazo na Taasisi za Umma, kuendelea kuwepo na kaya maskini, ushirikiano mdogo wa wananchi katika suala la utoaji wa ushahidi mahakamani dhidi ya watuhumiwa wa rushwa; kukosekana kwa sheria ya kuwabana wahusika

wanaoshindwa kutekeleza ushauri wa TAKUKURU kuziba mianya ya rushwa katika maeneo yao; na Mabadiliko ya TEHAMA yamekuwa yakiibua changamoto katika upeletelezi.

OFISI YA RAIS, IKULU NA TAASISI ZAKE

a. Ofisi ya Rais - Ikulu

62. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka wa Fedha 2020/21, Ofisi ya Rais, Ikulu imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Kutoa huduma kwa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na familia yake;
- (ii) Kutoa ushauri kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu ratiba ya kila siku;
- (iii) Kutoa ushauri kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika masuala ya Siasa, Uchumi, Jamii, Sheria, Diplomasia, Mawasiliano na Habari, Uhusiano wa Kikanda, Kimataifa na ushauri mwingine kwa lengo la kumsaidia Rais kufanya maamuzi;
- (iv) Kuratibu, kuandaa na kushiriki mikutano 60 ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, mikutano 40 ya Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu (IMTC) na mikutano 20 ya Baraza la Mawaziri;
- (v) Kuandaa mukutano wa tathmini wa mwaka kati ya Waratibu wa Shughuli za Baraza la Mawaziri wa

Wizara, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na wadau wengine;

- (vi) Kutoa mafunzo kuhusu utayarishaji na uwasilishaji wa Nyaraka za Baraza la Mawaziri na uchambuzi wa sera kwa Maofisa wa Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na Waratibu wa Shughuli za Baraza la Mawaziri wa Wizara;
- (vii) Kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu kwa kushirikisha wadau wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi;
- (viii) Kufanya mafunzo na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu (NACSAP III) na Programu za Maboresho katika ngazi za Wizara, Mikoa na Serikali za Mitaa;
- (ix) Kuandaa Taarifa za Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu, na kukamilisha mfumo wa kielektroniki wa Ufuatiliaji na Tathmini wa utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu (NACSAP III);
- (x) Kupokea, kupitia na kuchambua rufaa na malalamiko ya watumishi wa umma na wananchi;
- (xi) Kuendesha mikutano miwili ya Watendaji na Maafisa wa Serikali kuhusu utaratibu wa kushughulikia malalamiko na rufaa pamoja na

kufuatilia utekelezaji wa maagizo mbalimbali ya Katibu Mkuu Kiongozi;

- (xii) Kuratibu na kuendesha mikutano sita ya uratibu wa Maboresho kwa Makatibu Wakuu na Waratibu wa Programu za Maboresho kwa lengo la kuimarisha usimamizi, uongozi na umiliki wa mchakato wa Maboresho katika Sekta ya Umma nchini;
- (xiii) Kuratibu na kusimamia Miradi ya Maendeleo ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) na Programu ya Kujenga Uwezo wa Taasisi za Serikali Kupambana na Rushwa (BSAAT);
- (xiv) Kuendelea na uboreshaji wa Ikulu ya Chamwino; na
- (xv) Kukarabati majengo ya Ikulu ya Dar es salaam na Ikulu Ndogo za Mwanza, Arusha, Lushoto, Tabora na Shinyanga na nyumba za wafanyakazi zilizopo Dodoma.

b.TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA (TAKUKURU)

63. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka wa Fedha 2020/21, TAKUKURU imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Kukamilisha uchunguzi wa majalada ya tuhuma za rushwa unaoendelea pamoja na tuhuma mpya zitakazojitokeza;
- (ii) Kuendesha kesi 649 zinazoendelea na kesi mpya zitakazofunguliwa Mahakamani;
- (iii) Kufuatilia na kudhibiti vitendo vya rushwa kabla, wakati na baada ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 ili kuwadhibiti wagombea wote ambao sio waadilifu kwa kuhakikisha kuwa hawatumii fedha kuwarubuni wananchi kupata uongozi;
- (iv) Kuhuisha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya Mwaka 2007;
- (v) Kufanya utafiti kuhusu mianya ya rushwa katika sekta za umma na binafsi;
- (vi) Kufanya uchambuzi wa mifumo katika sekta na idara mbalimbali katika ngazi ya mikoa na wilaya;
- (vii) Kuweka mikakati kwa kushirikiana na wadau ili kudhibiti mianya ya rushwa na kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mikakati hiyo;
- (viii) Kufuatilia matumizi ya fedha za umma katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili

kuhakikisha utekelezaji wake unazingatia thamani halisi ya fedha;

- (ix) Kutekeleza Mkakati wa Mawasiliano wa TAKUKURU ili kujenga uwezo na uelewa kuhusu rushwa, ujisadi na juhudini za Serikali katika kupambana na rushwa kwa makundi mbalimbali katika jamii kwa kutumia njia mbalimbali za mawasiliano kuyashawishi makundi haya kuunga mkono na kushiriki katika mapambano dhidi ya rushwa nchini;
- (x) Kutumia njia za mawasiliano za kimkakati kulifikia kundi la vijana ili washiriki katika shughuli zinazowajenga kimaadili na kushiriki kupambana na rushwa ili kuwa na jamii inayochukia rushwa;
- (xi) Kutumia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kubeba agenda ya mapambano dhidi ya rushwa ili kuushirikisha umma katika mapambano hayo;
- (xii) Kujenga majengo ya ofisi za TAKUKURU katika mikoa na wilaya;
- (xiii) Kujenga karakana kwa ajili ya kutengeneza magari ya taasisi ili kupunguza gharama za uendeshaji zinazotumika katika kutengeneza magari hayo;

- (xiv) Kuimarisha mfumo wa TEHAMA katika taasisi ili kurahisisha na kuwezesha mtiririko mzuri wa majalada, takwimu na mawasiliano kutoka ngazi za wilaya, mkoa na makao makuu; na
- (xv) Kutoa mafunzo ya weledi kwa watumishi ili kuongeza ufanisi.

c. TAASISI YA UONGOZI

64. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka wa Fedha 2020/21, Taasisi ya UONGOZI imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Kutoa mafunzo ya Stashahada ya Uzamili ya Uongozi kwa lengo la kuwajengea uwezo Viongozi 35 katika maeneo ya kufanya maamuzi ya kimkakati, kusimamia rasilimaliwatu na rasilimali nyingine na kuimarisha sifa binafsi za kiongozi;
- (ii) Kutoa mafunzo ya Stashahada ya Uongozi kwa njia ya mtandao kwa Viongozi 30;
- (iii) Kutoa mafunzo ya muda mfupi kupitia kozi 30 kwa lengo la kuwajengea uwezo Viongozi 765 katika maeneo ya Uongozi na Maendeleo Endelevu, kutokana na mahitaji na maombi ya walengwa;
- (iv) Kuandaa mukutano wa kimataifa na kikanda na mikutano saba ya kitaifa katika masuala ya Uongozi na Maendeleo Endelevu;

- (v) Kuandaa vipindi 12 vya runinga vitakavyoshirikisha viongozi waandamizi na wataalam mbalimbali ndani na nje ya nchi, juu ya Uongozi na Maendeleo Endelevu. Vipindi hivi vitarushwa kwenye runinga, tovuti na mitandao ya kijamii na kuonekana katika Bara zima la Afrika;
- (vi) Kufanya utafiti kwenye maeneo manne kuhusu masuala ya Uongozi na Maendeleo Endelevu; na
- (vii) Kutoa ushauri wa kitaalam katika maeneo yanayohusu masuala ya Uongozi na Maendeleo Endelevu pale utakapohitajika.

d. MPANGO WA KURASIMISHA RASILIMALI NA BIASHARA ZA WANYONGE TANZANIA (MKURABITA)

65. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka wa Fedha 2020/21, MKURABITA imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Kuanzisha vituo saba vya urasimishaji na uendelezaji biashara ili kuwawezesha wafanyabishara kupata huduma muhimu sehemu moja katika Mamlaka za Serikali za Mitaa za Ilala, Mbeya, Iringa, Tunduma, Arusha, Musoma na Chato. Aidha, mafunzo ya kurasimisha na kuendesha biashara yatatolewa

- kwa wafanyabishara 4,900 kwa lengo la kuwawezesha kusajili biashara zao;
- (ii) Kuanzisha vituo vitatu vya urasimishaji wa biashara Zanzibar, katika Manispaa ya Chakechake, Mkoani na Kaskazini B ili kuwawezesha wafanyabiashara kupata huduma muhimu sehemu moja ambapo wafanyabiashara 1,500 watapata mafunzo na kusajili biashara zao;
 - (iii) Kutoa mafunzo kuhusu fursa na matumizi bora ya Hati za Haki Milki za Kimila kwa wakulima 1,500 waliorasimisha ardhi zao na viongozi 60 wa vyama vya wakulima katika Halmashauri za Wilaya Tatu za Chamwino, Kilolo na Kilosa. Aidha, kwa upande wa Zanzibar mafunzo yatatolewa kwa wamiliki 2,000 wa ardhi katika maeneo ya Nungwi, Welezo, Chokocho na Kiungoni;
 - (iv) Kukamilisha urasimishaji wa ardhi mjini katika Mamlaka za Serikali za Mitaa za Miji ya Morogoro, Tunduma, Babati, Iringa, Arusha, Njombe na Miji Midogo ya Tandala na Ikonda Tanzania Bara. Kwa upande wa Zanzibar, urasimishaji wa ardhi mjini utafanyika Chakechake na Unguja Mjini. Jumla ya Hati Milki 6,500 zitaandaliwa na kutolewa;

- (v) Kukamilisha uandaaji na utoaji Hati za Haki milki za Kimila 11,700 kwa wananchi katika Halmashauri za Wilaya za Rufiji, Kibiti, Musoma, Butiama, Chamwino, Nyang'wale, Makete, Bukoba Vijijini na Newala za Tanzania Bara. Aidha, kwa upande wa Zanzibar Hati Milki 2,000 zitatolewa katika maeneo ya Chanjamjawiri Wilaya ya Chakechake Pemba na Mahonda Wilaya ya Kaskazini B Unguja;
- (vi) Kukamilisha ujenzi wa Masjala za Ardhi za Vijiji katika Halmashauri za Wilaya nne za Chamwino (vijiji viwili), Itigi (kijiji kimoja), Mbinga (kijiji kimoja), Mvomero (kijiji kimoja). Aidha, ujenzi wa Masjala za Ardhi za vijiji utaanza katika Halmashauri za Wilaya ya Newala (kijiji kimoja) na Mbalali (kijiji kimoja);
- (vii) Kuendelea na urasimishaji wa Wachimbaji Wadogo wa Madini katika Mkoa wa Geita;
- (viii) Kufanya Ufutiliaji na Tathmini ya Utekelezaji wa shughuli za Urasimishaji ardhí katika Halmashauri za Mtwara, Magu, Mvomero, Chamwino, Korogwe, Serengeti, Uyui, Sikonge, Unguja na Pemba. Aidha, ufutiliaji na tathmini utafanyika kwa ajili ya urasimishaji wa biashara katika Halmashauri za Mtwara, Geita, Morogoro, Tanga, Babati, Tabora na Singida;

- (ix) Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya maboresho ya sheria za ardhi na biashara katika Wizara za Kisekta; na
- (x) Kuandaa vipindi 20 vya redio na runinga kuhusu utekelezaji wa Shughuli za urasimishaji Tanzania Bara na Zanzibar.

e. MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII (TASAF)

66. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka wa Fedha 2020/21, TASAF imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Kufanya utambuzi na uandikishaji wa kaya maskini katika maeneo ya Vijiji 2,072 na Mitaa 1,264 ambayo haikufikiwa katika kipindi cha kwanza cha Mpango. Zoezi hili linategemea kuzifikia kaya za walengwa zipatazo 235,647;
- (ii) Kufanya utambuzi na uhakiki wa hali za ustawi wa maisha ya walengwa wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini iwapo zimeboreka. Zoezi hili litatoa fursa ya kuwaondoa wale watakaobainika kuwa sio maskini tena kwa vigezo vitakavyotumika kupitia utaratibu wa wazi utakaoandaliwa na kukubalika na wadau katika maeneo husika;
- (iii) Kuhawilisha ruzuku kwa kaya maskini ambazo hazitakuwa na uwezo wa kufanya kazi katika Halmashauri 185 Tanzania Bara na wilaya zote Zanzibar;

- (iv) Kutoa ajira za muda kwa jumla ya kaya za walengwa 230,000 ambazo zitahusika katika utekelezaji wa miradi 2,500 ya kutoa ajira za muda itakayoibuliwa na jamii. Walengwa hawa watatoka katika Halmashauri 44 pamoja na Unguja na Pemba;
- (v) Kuendeleza utekelezaji wa Mkakati na Miongozo ya Kuweka Akiba na Kuwekeza Katika maeneo ya utekelezaji. Wawezeshaji 1,800 katika Halmashauri 72 watapatiwa mafunzo ya kuunda vikundi endelevu vyta kuweka akiba kwa kaya za walengwa. Jumla ya vikundi 21,600 vyta walengwa vitaundwa, kupewa mafunzo na vitendea kazi;
- (vi) Miradi 2,390 katika sekta ya afya, elimu, maji, ujasiriamali na barabara za vijiji itatekelezwa chini ya mpango wa kutoa ajira za muda katika Halmashauri 42 pamoja na Unguja na Pemba;
- (vii) Kutoa mafunzo ya namna ya kutekeleza na kusimamia miradi kwa wafanyakazi 6,984 wa Halmashauri na viongozi wa vijiji pamoja na kamati za usimamizi za jamii 24,444;
- (viii) Kuongeza wigo kwenye mfumo wa malipo ya walengwa kwa njia ya Kielektroniki (kupitia mitandao ya simu na Benki). Njia hii ya malipo itawezesha fedha kutumwa moja kwa moja kwa mlengwa na kumfikia kwa haraka ambapo

gharama za uendeshaji zitapungua kwa kiasi kikubwa;

- (ix) Kuimarisha mifumo ya TEHAMA ya utunzaji wa kumbukumbu za walengwa, uendeshaji na utoaji wa taarifa ili kuwezesha utekelezaji wa shughuli za Mpango hususan kuimarisha mawasiliano katika ya maeneo ya utekelezaji na TASAF Makao Makuu Dodoma;
- (x) Kujenga uwezo wa watumishi katika ngazi mbalimbali za utekelezaji ikiwa ni pamoja na TASAF Makao Makuu, wataalam wa sekta kutoka kwenye wizara, mikoa, halmashauri na jamii ili kuweza kusimamia na kutekeleza shughuli za Mpango kwa ufanisi;
- (xi) Kuimarisha usimamizi, ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za Mpango pamoja na matumizi ya rasilimali ili kuongeza ufanisi na uwajibikaji katika ngazi zote za utekelezaji wa Mpango; na
- (xii) Kufanya mapitio ya pamoja baina ya Timu ya Serikali na Wadau wa Maendeleo kuhusu maendeleo ya utekelezaji wa shughuli za Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini.

f. WAKALA YA NDEGE ZA SERIKALI

67. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka wa Fedha 2020/21, Wakala ya Ndege za Serikali imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Kutoa huduma ya usafiri wa anga kwa viongozi wakuu wa kitaifa;
- (ii) Kusimamia mikataba ya ukodishaji wa ndege kwa Kampuni ya Ndege ya Taifa (ATCL);
- (iii) Kufanya matengenezo makubwa ya ndege zinazowahudumia viongozi wakuu wa kitaifa na ununuzi wa vipuri vyta ya ndege za Serikali;
- (iv) Kufanya ukarabati wa karakana ya ndege za Serikali;
- (v) Kulipia gharama za bima za ndege;
- (vi) Kugharamia uendeshaji wa Ofisi na kulipia gharama za mafuta ya ndege; na
- (vii) Kutoa mafunzo kwa wanahe wa yanayohusu uhuishaji wa leseni zao.

68. *Mheshimiwa Spika*, ili kutekeleza Mpango wa Mwaka wa Fedha wa 2020/21, Fungu 20 Ofisi ya Rais, Ikulu inaomba kiasi cha **Shilingi 24,049,003,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Aidha, Fungu 30: Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri inaomba kiasi cha **Shilingi 608,155,446,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo.

Kati ya fedha hizi, **Shilingi 439,935,875,000** ni Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 168,219,571,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

69. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka wa Fedha 2020/21, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kama ifuatavyo:-

- (i) Kupokea Matamko ya Viongozi wa Umma kuhusu Rasilimali na madeni yanayopaswa kutolewa kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma;
- (ii) Kupokea na kushughulikia malalamiko na taarifa za ukiukwaji wa maadili kutoka kwa wananchi kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma;
- (iii) Kuchunguza tuhuma za ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma dhidi ya Viongozi wa Umma;
- (iv) Kufanya uhakiki wa matamko ya Rasilimali na Madeni kwa Viongozi wa Umma 2,000;
- (v) Kuratibu na kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Baraza la Maadili ya Viongozi wa Umma;

- (vi) Kutoa elimu kwa Viongozi wa Umma na wananchi kuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Hati ya Ahadi ya Uadilifu;
- (vii) Kuandaa taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa shughuli za Sekretarieti na kuiwasilisha kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
- (viii) Kufanya utafiti kuhusu hali ya Mgongano wa Maslahi mionganoni mwa Viongozi wa Umma;
- (ix) Kuanzisha na kuendeleza Klabu za Maadili katika shule na vyuo nchini;
- (x) Kuendelea na ujenzi wa Ofisi ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma Makao Makuu Dodoma; na
- (xi) Kuimarisha mifumo ya mawasiliano katika kutumia mfumo wa ujazaji wa fomu za matamko ya rasilimali na madeni kwa viongozi wa umma kwa njia ya mtandao kwa kuunganisha mfumo na mifumo mingine ya Serikali.

70. *Mheshimiwa Spika*, katika kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha wa 2020/21, Fungu 33: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma inaomba kuidhinishiwa **Shilingi 9,471,110,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizi, **Shilingi 7,621,110,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na

Shilingi 1,850,000,000 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA TAASISI ZILIZO CHINI YAKE

a. Menejimenti ya Utumishi wa Umma

71. *Mheshimiwa Spika*, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma katika Mwaka wa Fedha 2020/21 itaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kuhakikisha kuwa Utumishi wa Umma unaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora na kwamba Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu mbalimbali za Utumishi wa Umma zinazingatiwa. Aidha, Ofisi itahakikisha watumishi wa Umma wanawajibika na kuwa wasikivu kwa wananchi wanapotoa huduma mbalimbali.

72. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka wa Fedha 2020/21, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Kujenga uwezo wa Taasisi za Serikali katika kuandaa Sera za Kisekta zinazozingatia utafiti ili kuziwianisha na kuondoa migongano na urudufu wakati wa utekelezaji;
- (ii) Kufanya mapitio ya Sheria na Miongozo ya kiutumishi katika Utumishi wa Umma kwa lengo la kuboresha utendaji kazi;

- (iii) Kuhuisha miundo ya Maendeleo ya Utumishi na kuwianisha na kuoanisha viwango vya mishahara katika Utumishi wa Umma kwa kuzingatia matokeo ya zoezi la Tathmini ya Kazi;
- (iv) Kufanya ufuatiliaji na kuhamasisha ujumuishwaji wa masuala ya Anuai za Jamii katika Utumishi wa Umma ili kutoa huduma bora kwa wananchi;
- (v) Kutoa miongozo ya kuimarisha Menejimenti ya Utumishi Umma kupitia Nyaraka za Kiutumishi;
- (vi) Kushughulikia mahitaji ya vibali vya uhamisho, kushikizwa, kuazimwa na likizo bila malipo kwa watumishi na baina ya waajiri mbalimbali katika Utumishi wa Umma;
- (vii) Kupokea na kushughulikia mapendekezo ya nafasi za uteuzi, mikataba ya ajira na vibali vya kukaimu nafasi za uongozi kadiri maombi hayo yatakavyokuwa yanawasilishwa na waajiri mbalimbali;
- (viii) Kuelimisha watumishi wa Umma na waajiri kuhusu umuhimu wa kupunguza malalamiko ya wateja na kushughulikia ipasavyo malalamiko yanayowasilishwa;
- (ix) Kuimarisha upatikanaji wa taarifa (Kanzi data) za Viongozi wa Serikali, Maafisa Waandamizi na Maafisa Daraja I;

- (x) Kusimamia ajira za watumishi wa Umma ambapo katika Mwaka wa Fedha 2020/21 Serikali inatarajia kuajiri watumishi wapya 44,811 wakiwemo wa Kada ya Elimu (13,529), Afya (10,467), Kilimo, Mifugo na Uvuvi (2,145) Jeshi la Polisi (2,725), Magereza (685), Jeshi la Zimamoto (501), Uhamiaji (495) na Hospitali za Mashirika ya Kidini na hiari (1,262). Aidha, Serikali inatarajia kuajiri watumishi 13,002 wa Kada nyinginezo wakiwemo wahadhiri wa vyuo vikuu vya Umma nchini;
- (xi) Kupandisha vyeo watumishi 222,290 wa Kada mbalimbali kulingana na maelekezo yatakayotolewa;
- (xii) Kuchambua na kuhakiki madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi wa Umma 20,027 yenye thamani ya **Shilingi 45,743,803,190.79** na kuchukua hatua ipasavyo;
- (xiii) Kuidhinisha taarifa za kiutumishi na mishahara kwenye Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS);
- (xiv) Kufanya uhakiki wa watumishi kwenye Sekretarieti za Mikoa ili kuhakikisha kunakuwa na matumizi bora ya rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma;
- (xv) Kuhakikisha kuwa taarifa za watumishi zinakuwa sahihi na kuboresha taarifa za kiutumishi na mishahara kupitia HCMIS;

- (xvi) Kuendesha mafunzo ya namna ya kutumia Mfumo mpya wa HCMIS kwa watumishi wa umma;
- (xvii) Kuhuisha miundo na mgawanyo wa majukumu ya Ofisi/Wizara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali na Mashirika ya Umma 100 na kuziwasilisha kwa Mheshimiwa Rais kwa ajili ya kupata idhini ya utekelezaji. Lengo la shughuli hii ni kuongeza ufanisi katika utoaji huduma pamoja na kupunguza ukubwa na matumizi ya Serikali ili fedha zitakazopatikana zielekezwe kwenye miradi ya maendeleo;
- (xviii) Kuwezesha Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali na Mashirika ya Umma 20 kuandaa Orodha ya Kazi na Maelezo ya Kazi ili kupata uwiano mzuri wa watumishi katika kutekeleza majukumu ya Taasisi husika;
- (xix) Kuboresha michakato ya utoaji huduma na kuimarisha usimamizi wa Mifumo na Viwango vya utendaji kazi kwa kufanya ufuatiliaji pamoja na kutoa ushauri wa kitaalam katika Taasisi za Serikali ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wananchi;
- (xx) Kuandaa Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Kitaifa na kuwezesha utekelezaji wake;
- (xxi) Kuandaa Mfumo Jumuishi wa Ufuatiliaji na Tathmini Serikalini kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ambao utaunganisha Mifumo ya

Ufutiliaji na Tathmini iliyopo katika Taasisi zote za Umma;

- (xxii) Kuratibu fursa za mafunzo yanayotolewa na Serikali na Wadau wa Maendeleo;
- (xxiii) Kuwezesha Taasisi za Umma 10 kuandaa Mipango ya Rasilimaliwatu, Mipango ya Mafunzo na Urithishanaji wa madaraka;
- (xxiv) Kukamilisha na kusambaza Mwongozo wa Kuwezesha Taasisi za Umma Kuandaa Mpango wa Rasilimaliwatu wa muda wa kati na muda mrefu;
- (xxv) Kuandaa Mfumo wa Kielektroniki wa Mpango wa Rasilimaliwatu;
- (xxvi) Kukamilisha mapitio ya Kanuni za Maadili ya Utumishi wa Umma na kujenga uelewa wa Kanuni hizo kwa wadau;
- (xxvii) Kufanya Ufutiliaji wa Uzingatiaji wa Maadili katika Sekretarieti za Mikoa miwili, Mamlaka za Serikali za Mitaa 10 na Taasisi nyingine za Umma tano;
- (xxviii) Kuwezesha uanzishwaji wa Mfumo wa Kushughulikia Malalamiko ya Wananchi katika Utumishi wa Umma kwenye Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na Taasisi nyingine za Umma;

- (xxix) Kufanya kampeni za kimaadili kwenye Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- (xxx) Kufanya uhamasishaji wa uzingatiaji wa maadili kuitia vyombo vya habari;
- (xxxi) Kushughulikia malalamiko ya wananchi yanayohusu ukiukwaji wa maadili katika Utumishi wa Umma;
- (xxxii) Kuhimiza na kusimamia uanzishwaji wa Kamati za Uadilifu katika Taasisi za Umma;
- (xxxiii) Kuratibu uanzishwaji wa vituo vya HUDUMA PAMOJA kwa ajili ya kutolea Huduma za Serikali sehemu moja;
- (xxxiv) Kufanya tathmini na kuwajengea uwezo wataalamu wa TEHAMA katika taasisi za Serikali ili kuwawezesha kujenga, kusimamia na kuendeleza mifumo ya TEHAMA ya Serikali;
- (xxxv) Kufuatilia uzingatiaji wa mwongozo wa kusimamia utekelezaji wa Serikali Mtandao ya Mwaka 2017 katika taasisi za Serikali;
- (xxxvi) Kufanya ukaguzi wa usalama wa mifumo ya HCMIS na e-OPRAS;
- (xxxvii) Kujenga uwezo kwa Maafisa TEHAMA na watumishi wengine kuhusiana na Mkakati wa Matumizi ya TEHAMA;
- (xxxviii) Kukamilisha maandalizi ya Mpango Mkakati wa Taifa wa utekelezaji wa Serikali Mtandao;

- (xxxix) Kuratibu maandalizi ya Kanuni mbalimbali za utekelezaji wa Sheria inayotungwa ya Serikali Mtandao;
- (xli) Kuratibu maandalizi na utekelezaji wa Programu ya Dijitali Tanzania;
- (xlii) Kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Sera ya Usalama ya Kielektroniki;
- (xlii) Kufanya Tathmini ya kina ya Utendaji kazi wa Wakala za Serikali;
- (xlvi) Kujenga uelewa wa Viongozi wa Kisiasa na Watendaji katika Taasisi za Umma, Menejimenti na watumishi kuhusu Mikataba ya Utendaji Kazi Serikalini;
- (xliii) Kuziwezesha Taasisi za Umma kuandaa na kutekeleza Mikataba ya Utendaji Kazi;
- (xlv) Kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mfumo wa Wazi wa Mapitio na Tathmini ya Utendaji Kazi (OPRAS) kwenye Taasisi za Umma;
- (xlii) Kufanya mkutano wa ufuatiliaji na wadau kuhusu majoribio ya utekelezaji wa Mfumo wa Wazi wa Mapitio na Tathmini ya Utendaji Kazi wa Kielektroniki (e - OPRAS);
- (xlvii) Kuwezesha usimamizi, uwekaji na mafunzo ya Mfumo wa Wazi wa Mapitio na Tathmini ya Utendaji Kazi wa Kielektroniki (e - OPRAS) kwa taasisi za umma;

- (xlviii) Kuendelea kutoa huduma za kitaalamu katika Usimamizi wa Mikataba ya Utendaji kazi kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Mashirika ya Umma, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- (xlix) Kutekeleza shughuli za Programu ya Maboresho katika Utumishi wa Umma kwenye maeneo ya matokeo ya Motisha na Uwajibikaji; Michakato ya Utoaji Huduma; na Menejimenti ya Rasimaliwatu;
- (I) Kutoa elimu kuhusu majukumu ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora;
- (ii) Kutoa mafunzo kwa Watumishi wa Umma wanaotarajiwa kustaa fu mwaka 2020/21 ili kuwaandaa kwa maisha ya baada ya miaka ya ajira katika Utumishi wa Umma;
- (iii) Kujenga nyumba 500 katika mikoa mbalimbali ikiwemo nyumba 300 jijini Dodoma;
- (iv) Kuanzisha Mfuko wa Uwekezaji wa "Faida Fund" ambao utawawezesha wafanyakazi, wakulima, wavuvi, wafugaji, wafanya biashara wadogo na wanafunzi kuweka akiba kwa njia ya kununua vipande na kukuza mitaji yao kupitia uwekezaji wenye faida;
- (iv) Kutoa huduma ya upimaji ardhi kwa kushirikiana na halmashauri na taasisi za Serikali zenyenye uhitaji; na

- (iv) Kutoa huduma kwa Viongozi Wakuu wa Kitaifa (Wastaafu 11 na wajane 5) kwa mujibu wa sheria.

b. Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC)

73. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka wa Fedha 2020/21 Chuo kinatarajia kutekeleza malengo yafuatayo:-

- (i) Kutoa mafunzo ya kijiandaa kufanya mitihani ya Utumishi wa Umma kwa watumishi 1,115;
- (ii) Kutoa mafunzo ya lazima na yanayoombwa na Taasisi za Umma katika kukidhi mahitaji halisi ya watumishi wa umma kulingana na kada zao;
- (iii) Kutoa mafunzo yanayoendeleza stadi, weledi na ujuzi wa watumishi wa umma katika masuala ya Uongozi, Menejimenti, Utawala na uendeshaji wa ofisi za Umma kwa Watumishi wa Umma 3,920;
- (iv) Kutoa Mafunzo ya Awali katika Utumishi wa Umma kwa watumishi wa Umma 2,540;
- (v) Kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa washiriki 13,014 katika fani za Utunzaji wa Kumbukumbu, Uhazili, Kompyuta, Utunzaji wa Fedha za Umma, Menejimenti ya Rasilimaliwatu, Usimamizi wa Ununuzi wa Umma na Uongozi na Utawala Bora;

- (vi) Kutoa ushauri wa kitaalam katika maeneo 12 yatakayota fursa kwa watumishi wa umma kuboresha mifumo na mbinu za utekelezaji wa majukumu yao kwa mujibu wa mahitaji halisi ya utumishi wa umma na wadau mbalimbali kwa lengo la kukuza na kuendeleza uchumi wa Taifa letu;
- (vii) Kufanya utafiti wa mahitaji halisi ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma na kusambaza matokeo ya utafiti huo kwa lengo la kukuza weledi na ufanisi wa utendaji kazi kwa watumishi wa umma;
- (viii) Kuwezesha mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi nane wa Chuo cha Utumishi wa Umma katika ngazi zifuatazo; watumishi watano Shahada ya Uzamivu na watatu Shahada ya Uzamili;
- (ix) Kuanza ujenzi wa majengo yatakayotumika kwa ajili ya madarasa, maktaba na ofisi katika Kampasi za Singida na Tanga;
- (x) Kuandaa michoro ya usanifu majengo kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa majengo ya Kampasi ya Mwanza eneo la Luchelele;
- (xi) Kutafuta eneo kwa ajili ya ujenzi wa Kampasi ya Mbeya;

- (xii) Kutoa mafunzo yanayotoa fursa kwa watumishi wa Umma kuongeza stadi, weledi na ujuzi katika matumizi ya Teknolojia;
- (xiii) Kutoa mafunzo yanayolenga kubadilishana uzoefu kuhusu utawala na menejiementi ya utumishi wa Umma kwa mujibu wa mahitaji halisi ya utumishi wa Umma na wadau wengineo;
- (xiv) Kutoa mafunzo kwa watumishi wa Umma yanayolenga kuwaunganisha na kubadilishana uzoefu wa wataalamu wa kimataifa katika matumizi ya mifumo ya mawasiliano kwa njia ya mtandao katika utoaji wa huduma ndani na nje ya nchi;
- (xv) Kuendesha mafunzo kwa njia ya mtandao ili kusaidia Serikali kupunguza gharama, kuwa na mazingira rafiki katika kujifunza, kutoa fursa ya kuepuka muingiliano wa mafunzo na majukumu ya kazi, kupunguza safari nje ya mahali pa kazi na kuepuka kuwa mbali na familia; na
- (xvi) Kukuza Sera za Serikali za utamaduni wa kujifunza na kusaidia utumiaji wa Teknolojia miongoni mwa watendaji katika kutelekeza majukumu yao kwa lengo la kukuza uchumi na kuleta maendeleo nchini.

c. Mamlaka ya Serikali Mtando (e-GA)

74. *Mheshimiwa Spika*, Katika Mwaka wa Fedha 2020/21, Mamlaka ya Serikali Mtando inatarajia kutekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Kusanikisha katika taasisi za umma, Mfumo Shirikishi wa Kusimamia Shughuli na Rasilimali za Taasisi;
- (ii) Kuhuisha na kutekeleza Mifumo Shirikishi ya TEHAMA ikiwemo Mfumo wa Kutoa Huduma kwa Njia ya Simu za Mkononi kwa Taasisi za Umma; Mfumo wa Vibali vya Kusafiria Nje ya Nchi, Mfumo wa Masijala na Mfumo wa Barua Pepe wa Serikali;
- (iii) Kuendelea na uimarishaji wa usalama wa mifumo ya TEHAMA;
- (iv) Kuwezesha mifumo ya TEHAMA ya kimkakati na ya kisekta kubadilishana taarifa;
- (v) Kuimarisha Vituo vya Kuhifadhi Taarifa na Mifumo ya TEHAMA ya Serikali na Kujikinga na Majanga ili kuongeza usalama wa mifumo na taarifa za Serikali na kupunguza gharama ya kuhifadhi rasilimali shirkishi mionganini mwa Taasisi za Umma;
- (vi) Kusimamia na kuimarisha usalama wa Mtando wa Mawasiliano Serikalini;

- (vii) Kutoa mafunzo ya Serikali Mtandao kwa Viongozi, Wasimamizi wa TEHAMA na watumiaji wa huduma za Serikali Mtandao kwa Taasisi za Serikali ili kuongeza uelewa na uwezo wa Taasisi za Umma katika kutumia TEHAMA na kuongeza ufanisi wa kiutendaji na utoaji wa huduma kwa wananchi;
- (viii) Kutoa ushauri wa kitaalam na msaada wa kiufundi kwa taasisi za Umma katika utekelezaji wa serikali mtandao;
- (ix) Kutoa elimu kwa Umma kuhusu utekelezaji wa sheria ya serikali mtandao pamoja na sheria na kanuni zake; na
- (x) Kuwajengea uwezo watumishi wa mamlaka kwa kuwapatia mafunzo mbalimbali yanayoendana na taaluma zao ili kuboresha utekelezaji wa majukumu yao ya kazi.

75. *Mheshimiwa Spika*, ili kutekeleza Mpango wa Mwaka wa Fedha wa 2020/21, Fungu 32 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma inaomba kiasi cha **Shilingi 43,878,828,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizi, **Shilingi 32,923,578,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 10,955,250,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA

76. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka wa Fedha 2020/21, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

- (i) Kusimamia na kuendesha michakato ya ajira ili kuwezesha waajiri kupata watumishi wenye sifa zinazotakiwa kwa mujibu wa miundo ya utumishi husika;
- (ii) Kushiriki kama wataalam waalikwa kwenye usaili unaoendeshwa na taasisi zinazotumia Sheria zilizokasimiwa kwa taasisi husika;
- (iii) Kuimarisha Ofisi ya Sekretarieti ya Ajira iliyopo Zanzibar ili kurahisisha michakato ya ajira kwa ajira za Muungano;
- (iv) Kuhamisha watumishi wa Ofisi kutoka Dar es Salaam kwenda Makao Makuu Dodoma;
- (v) Kufanya utafiti kwa waajiri na wadau mbalimbali ikiwa ni hatua ya kupata mrejesho wa utekelezaji wa shughuli za uendeshaji wa michakato ya ajira pamoja na utendaji kazi wa Ofisi;
- (vi) Kuimarisha utendaji kazi wa taasisi kwa kutumia TEHAMA;
- (vii) Kuboresha mifumo ya uendeshaji wa usaili kwa kutumia mbinu za kisasa, ikiwemo matumizi ya “psychometric test”;

- (viii) Kutoa taarifa na elimu kwa Umma ili kukuza uelewa kuhusu shughuli zinazoteklezwa na Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma;
- (ix) Kuhakiki vyeti vya waombaji kazi na kupata taarifa nyingine muhimu ili kupunguza kesi zinazotokana na kugushiwa kwa vyeti; na
- (x) Ununuzi wa vitendea kazi hususani magari ili kusaidia utekelezaji wa majukumu ya Taasisi kwa wakati.

77. *Mheshimiwa Spika*, katika kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha wa 2020/21, Fungu 67: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 3,360,526,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

OFISI YA RAIS, TUME YA UTUMISHI WA UMMA

78. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka wa Fedha 2020/21, Tume imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

- (i) Kukagua taasisi (Waajiri, Mamlaka za Ajira na Nidhamu) 160 katika Ukaguzi wa Kawaida na Ukaguzi Maalum kwa taasisi 10 ili kuangalia uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu za usimamizi wa Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma;

- (ii) Kufanya mikutano ya Kisheria ya Tume ili kujadili na kutolea uamuzi rufaa na malalamiko, taarifa za ukaguzi na masuala mengine ya kiutumishi kadri yatakavyopokelewa;
- (iii) Kuhuisha Miongozo ya Tume ya uzingatiaji wa masuala ya Ajira na Nidhamu na kuisambaza kwa Waajiri, Mamlaka za Ajira na Nidhamu;
- (iv) Kuelimisha taasisi za Umma na watumishi wa Umma kuhusu majukumu ya Tume na utekelezaji wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Utumishi wa Umma kuitia, ziara za Makamishna, vikao vya kazi, vyombo vya habari, machapisho na Tovuti;
- (v) Kuandaa Taarifa ya Hali ya Utumishi wa Umma na Utekelezaji wa Majukumu ya Tume kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2019/20 na kuiwasilisha kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
- (vi) Kutoa huduma kwa watumishi wa Tume wenye mahitaji maalum; na
- (vii) Kutoa elimu kwa watumishi wa Tume kuhusu VVU, UKIMWI, Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza na mapambano dhidi ya rushwa.

79. *Mheshimiwa Spika*, ili kutekeleza Mpango wa Mwaka wa Fedha 2020/21, Fungu 94, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 5,231,094,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

BODI YA MISHAHARA NA MASILAHİ KATIKA UTUMISHI WA UMMA

80. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka wa Fedha 2020/21, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma (Fungu 09) inatarajia kutekeleza majukumu kama ifuatavyo:-

- (i) Kufanya utafiti kuhusu utekelezaji wa Mfumo wa Jumla wa Kimenejimenti wa Motisha katika Utumishi wa Umma ili kuishauri Serikali juu ya mfumo huo;
- (ii) Kufanya utafiti kuhusu mazingira magumu ya kazi;
- (iii) Kuandaa taarifa ya gharama ya maisha kila robo mwaka na kushauri juu ya gharama za chini za maisha;
- (iv) Kukusanya na kuchambua taarifa za misingi ya kuzingatiwa katika kutoa masilahi na ushauri wa mwongozo wa kuzingatiwa wakati wa kutoa masilahi.

81. *Mheshimiwa Spika*, katika kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2020/21, Fungu 9: Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 1,445,945,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

OFISI YA RAIS, IDARA YA KUMBUKUMBU NA NYARAKA ZA TAIFA

82. *Mheshimiwa Spika*, kwa mujibu wa Sheria ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa Na. 3 ya mwaka 2002, Idara ya Kumbukumbu ya Nyaraka za Taifa imepewa jukumu la kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu za utunzaji kumbukumbu na nyaraka katika Taasisi za Umma. Aidha, Idara ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Kuwaenzi Waasisi wa Taifa Na. 18 ya Mwaka 2004 katika kukusanya, kutunza na kuhifadhi kumbukumbu na vitu vya Waasisi wa Taifa letu (Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume).

83. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka wa Fedha 2020/21, Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa itatekeleza shughuli zifuatazo:-

- (i) Kukusanya taarifa, kumbukumbu, nyaraka na machapisho mbalimbali yanayohusu historia ya Nchi yetu kutoka taasisi za Umma, taasisi na watu binafsi;

- (ii) Kutambua, kukusanya, kutunza na kuhifadhi kumbukumbu na vitu vya Waasisi wa Taifa;
- (iii) Kuimarisha Vituo vya Kanda kwa lengo la kuongeza uwezo wa Idara katika ukusanyaji na utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka;
- (iv) Kuweka na kuhuisha mifumo ya utunzaji wa kumbukumbu katika Taasisi za Umma ili kuongeza ufanisi na tija katika utoaji wa huduma Serikalini;
- (v) Kuimarisha mifumo ya kielektroniki katika usimamizi wa taarifa, kumbukumbu na nyaraka za taifa kwa ajili ya kuhifadhi kumbukumbu na nyaraka katika teknolojia ya kisasa ili kurahisisha upatikanaji na kulinda nakala halisi;
- (vi) Kusaidia taasisi za umma kutengeneza miongozo ya kuhifadhi na kuteketeza kumbukumbu pamoja na kufanya tathmini ya kumbukumbu tuli za taasisi za umma zilizohifadhiwa katika Kituo cha Taifa cha Kumbukumbu Dodoma;
- (vii) Kujenga uwezo wa taasisi za Umma katika usimamizi wa kumbukumbu na nyaraka za Serikali kwa kuandaa mikutano kazi kwa menejimenti za taasisi za Umma na mafunzo kazi kwa Waratibu na Watunza kumbukumbu kuhusu Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya utunzaji wa taarifa, kumbukumbu na nyaraka za Serikali;

- (viii) Kutoa elimu kwa wananchi kuhusiana na umuhimu wa utunzaji na uhifadhi wa kumbukumbu na nyaraka za Taifa pamoja na shughuli za Idara; na
- (ix) Kuimarisha uwezo wa utendaji wa Watumishi wa Idara.

84. *Mheshimiwa Spika*, katika kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2020/21, Fungu 4: Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 4,564,368,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizi, **Shilingi 2,564,368,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 2,000,000,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

C. MAJUMUISHO

85. *Mheshimiwa Spika*, Kwa kuwa hii ni bajeti ya mwisho ya kipindi cha Awamu ya Tano, hatuna budi kujivunia mafanikio ambayo Ofisi yangu imeyapata. Miongoni mwa masuala ambayo Serikali ya Awamu ya Tano iliahidi kuyashughulikia ni suala la watumishi hewa na wenyewe vyeti feki ambapo watumishi wapatao 19,708 waliondolewa na kiasi cha **Shilingi Bilioni 19.84.** kwa mwezi kuokolewa.

86. *Mheshimiwa Spika*, Katika kipindi hiki, kodi ya Mshahara kwa watumishi wa Umma (PAYE) ilipunguzwa hadi tarakimu moja kwa kima cha chini kutoka asilimia 11 hadi asilimia 9 ikiwa ni utekelezaji wa ahadi za Ilani ya CCM ya Uchaguzi ya Mwaka 2015. Ofisi yangu pia, ilihakikisha kuwa nidhamu ya utendaji kazi na maadilli ya watumishi wa Umma vinaimarishwa. Vile vile, watanzania wameshuhudia jinsi masuala ya rushwa na uhujumu uchumi yalivyoshughulikiwa kwa mafanikio makubwa ili kulinda rasilimali za Umma.

87. *Mheshimiwa Spika*, Suala jingine ambalo Serikali ya Awamu ya Tano iliahidi kulisimamia ni suala la ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Ofisi yangu, kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango, imeimarisha na kujenga mifumo ukiwemo Mfumo Mkuu wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato Serikalini “Government e-Payment Gateway – GePG”. Mifumo hii imesaidia sana kurahisisha ukusanyaji wa mapato, kuziba mianya ya upotevu wa fedha za umma na kuwezesha ongezeko la ukusanyaji wa mapato katika sekta mbalimbali za Serikali kuanzia Serikali Kuu hadi Mamlaka za Serikali za Mitaa.

88. *Mheshimiwa Spika*, Katika kufanikisha ongezeko la matumizi ya Serikali Mtandao isiyokuwa na urudufu na kufanikisha azma ya Serikali ya kutumia Serikali Mtandao kwa asilimia 100 ifikapo Mwaka 2025, Ofisi yangu imewezesha utungwaji wa Sheria ya

Mamlaka ya Serikali Mtandao ili kuipa nguvu taasisi ya awali katika kuratibu, kusimamia na kukuza jitihada za Serikali mtandao.

89. *Mheshimiwa Spika*, Baada ya kueleza baadhi ya mafanikio turejee kuwa Utumishi wa Umma ni mtambuka na endelevu kwa maana ya menejimenti yake na utawala bora hivyo unatarajiwa kuendelea kuwa nguzo muhimu katika uendeshaji wa nchi katika kipindi cha mwaka 2020/21 na hivyo kutoa mchango mkubwa sana katika utulivu wa nchi yetu na maendeleo tunayodhamiria kuelekea kwenye nchi ya uchumi wa kipato cha kati ifikapo mwaka 2025. Aidha, maendeleo hayo yanatarajiwa kupatikana kwa kuimarisha uchumi wa viwanda kama inavyowekwa wazi katika Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

90. *Mheshimiwa Spika*, kama nilivyoeleza katika utangulizi wa Hotuba yangu, mwaka huu wa 2019/20, tunakamilisha kipindi cha Bunge la 11, hivyo hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa nguvu na afya katika kutekeleza majukumu yetu kwa kipindi chote. Aidha, sote tunatambua kuwa mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi Mkuu ambapo wengi wetu tunatarajia kwenda kwa wananchi kuomba ridhaa yao ya kuwawakilisha kwa miaka mingine mitano. Ninawaombea nyote kwa Mwenyezi Mungu ili sote tutakaogombea tena tushinde katika majimbo yetu kwa kishindo na hatimaye tuendelee kukamilisha kazi

iliyoanzishwa na Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Rais Dkt. John Joseph Pombe Magufuli.

91. *Mheshimiwa Spika*, kwa mujibu wa miundo na mgawanyo wa majukumu kwa mawaziri, utekelezaji wa Ofisi yangu kwa ujumla unajumuisha, Ofisi ya Rais Ikulu; Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma; Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma; Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma; Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma; na Ofisi ya Rais, Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa.

92. *Mheshimiwa Spika*, Mipango na Bajeti kwa Mafungu niliyoyataja yamezingatia vipaumbele vya Serikali ya Awamu ya Tano kwenye eneo la kuimarishe utendaji kazi wa Utumishi wa Umma na kuifanya nchi yetu iondokane na matumizi mabaya ya rasilimali fedha, ukiukwaji wa maadili ya uongozi na kupunguza urasimu usio wa lazima katika utoaji huduma na hivyo kuongeza tija katika kutekeleza masuala yenyе masilahi mapana kwa Taifa letu.

93. *Mheshimiwa Spika*, Bajeti ya Mafungu yote yaliyo chini ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imelenga kuwa na Utumishi wa Umma unaotoa huduma bora kwa haraka na staha, kuzingatia Katiba, Sera,

Sheria, Kanuni, Miongozo na taratibu ili kujenga imani zaidi kwa wananchi. Katika kuendana na wakati jitihada zaidi zitawekwa kwenye kujenga uwezo na mifumo ya kimenejimenti na utoaji huduma ikiwemo matumizi sahihi na salama ya fursa zinazopatikana katika utoaji huduma kwa TEHAMA ndani ya Serikali.

94. *Mheshimiwa Spika*, baada ya kueleza kwa kina utekelezaji wa majukumu kwa Mwaka wa Fedha 2019/20 na Mipango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2020/21, naomba sasa, kuwasilisha rasmi mapendekezo ya maombi ya Ofisi yangu kwa Mwaka wa Fedha 2020/21 kwa muhtasari kama ifuatavyo:-

a. Fungu 20: Ofisi ya Rais, Ikulu

i. Matumizi ya Kawaida Sh.	<u>24,049,003,000</u>
Jumla	Sh. <u>24,049,003,000</u>

b. Fungu 30: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri

i. Matumizi ya Kawaida Sh.	439,935,875,000
ii. Matumizi ya Miradi Sh.	<u>168,219,571,000</u>
ya Maendeleo	
Jumla	Sh. <u>608,155,446,000</u>

c.	Fungu 33: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma		
i.	Matumizi ya Kawaida Sh.	7,621,110,000	
ii.	Matumizi ya Miradi Sh. ya Maendeleo	<u>1,850,000,000</u>	
	Jumla	Sh.	<u>9,471,110,000</u>
d.	Fungu 32: Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma		
i.	Matumizi ya Kawaida Sh.	32,923,578,000	
ii.	Matumizi ya Miradi ya Maendeleo	Sh.	<u>10,955,250,000</u>
	Jumla	Sh.	<u>43,878,828,000</u>
e.	Fungu 67: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma		
i.	Matumizi ya Kawaida Sh.	<u>3,360,526,000</u>	
	Jumla	Sh.	<u>3,360,526,000</u>
f.	Fungu 94: Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma		
	Matumizi ya Kawaida	Sh.	<u>5,231,094,000</u>
	Jumla	Sh.	<u>5,231,094,000</u>

g. Fungu 09: Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma

Matumizi ya Kawaida	Sh.	<u>1,445,945,000</u>
Jumla	Sh.	<u>1,445,945,000</u>

h. Fungu 04: Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa

Matumizi ya Kawaida	Sh.	2,564,368,000
Matumizi ya Miradi ya Sh. Maendeleo		<u>2,000,000,000</u>
Jumla	Sh.	<u>4,564,368,000</u>

95. Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, Jumla kuu ya Bajeti ninayoomba kwa mafungu yote yaliyo chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2020/21, ni kama ifuatavyo:-

Matumizi ya Kawaida	Sh.	517,131,499,000
Matumizi ya Miradi ya Sh. Maendeleo		<u>183,024,821,000</u>
Jumla	Sh.	<u>700,156,320,000</u>

96. *Mheshimiwa Spika* na *Waheshimiwa Wabunge*, mwisho naomba kuwasilisha maombi haya ili muweze kuyajadili na kuyaidhinisha.

97. *Mheshimiwa Spika*, naomba kutoa hoja.

Kapt. (Mst.) George H. Mkuchika (Mb.)

WAZIRI WA NCHI – OFISI YA RAIS

**(MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA
UTAWALA BORA)**

**TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA
TAKWIMU ZA UCHUNGUZI KWA KIPINDI CHA JULAI 2019 - MACHI 2020**

MAELEZO	JUL	AGO	SEP	OKT	NOV	DES	JAN	FEB	MACH	JUMLA	
Malalamiko Yaliyopokelewa***	1,056	955	1,277	1,491	996	2,156	1,168	966	628	10,693	
Majalada yaliyokamiliika	76	74	122	184	99	178	78	62	64	937	
Majalada Yaliyopelekwa kwa DPP	10	22	7	26	0	25	14	37	42	183	
Majalada yaliyorudi na kibali cha DPP	1	12	6	0	0	11	10	1	6	47	
Majalada Yaliyofungwa	14	3	5	9	12	25	2	0	2	72	
Kesi Mpya Zilizofikishwa Mahakamani	25	31	36	47	43	61	37	36	36	352	
Kesi zilizoamuliwa Mahakamani	9	16	22	30	23	38	19	25	14	196	
Kesi Zilizoshindwa	3	7	27	19	11	48	7	9	12	143	
Kesi zinazoendela mahakamani	561	608	660	552	588	662	585	639	649	649	
Thamani ya Fedha Iliyookolewa (Tshs)	Fedha Taslimu	72,791,944	289,243,062	316,018,238	546,963,293	295,461,202	1,155,349,366	1,388,665,781	1,214,841,152	564,223,129	5,843,557,167
	Fedha zilizodhibitiwa	30,648,218,080	81,516,510	308,626,564	86,989,260	27,862,000	305,196,673	409,144,423	552,985,044	432,160,854	32,852,699,408

KIAMBATISHO NA. 2

MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII (TASAF)

**FEDHA ZA MALIPO KWA WALENGWA KWA MAENEKO YOTE YA UTEKELEZAJI PAMOJA NA FEDHA ZA
USIMAMIZI NGAZI YA MKOA HALMASHAURI KATA KIJJI/MTAA/SHEHIA KWA KIPINDI CHA KUANZIA JULAI
2019 HADI JANUARI 2020**

ENEO LA UTEKELEZAJI	IDADI YA VIJJJI/ MITAA/ SHEHIA	IDADI YA KAYA	MALIPO KWA WALENGWA	MALIPO YA USIMAMIZI NGAZI YA KIJJI/MTAA/ SHEHIA	MALIPO YA USIMAMIZ I NGAZI YA MKOA	MALIPO YA USIMAMIZI NGAZI YA WILAYA NA KATA		MALIPO YA AJIRA ZA MUDA		JUMLA YA FEDHA KILA HALMASHAURI
						WILAYA	KATA	IDADI YA WALENGWA	MALIPO KWA WALENGWA	
Arusha										
Arusha	45	9,102	288,076,000	4 500 000	1 350 000	11 798 715	675 000	0	0	306,399,715
Arusha Mjini	71	4,661	153,712,000	7 100 000	2 130 000	13 994 950	1 065 000	0	0	178,001,950
Karatu	39	7,398	266,464,000	3 900 000	1 170 000	12 486 795	585 000	0	0	284,605,795
Longido	27	5,639	202,784,000	2 700 000	810 000	14 300 670	405 000	0	0	220,999,670
Meru	47	5,484	180,180,000	4 700 000	1 410 000	12 038 580	705 000	0	0	199,033,580
Monduli	31	5,849	210,252,000	3 100 000	930 000	14 199 520	465 000	0	0	228,946,520
Ngorongoro	31	5,726	202,100,000	3 100 000	930 000	19 024 660	465 000	0	0	225,619,660
JUMLA NDOGO	291	43,859	1,503,568,000	29 100 000	8 730 000	97 843 890	4 365 000	0	0	1,643,606,890
Dar es Salaam										
Ilala	73	4,713	176,180,000	7 300 000	2 190 000	14 280 025	1 095 000	0	0	201,045,025
Kinondoni	114	6,804	231,744,000	11 400 000	3 420 000	18 908 530	1 710 000	0	0	267,182,530
Temeke	121	8,735	299,696,000	12 100 000	3 630 000	19 809 365	1 815 000	0	0	337,050,365
JUMLA NDOGO	308	20,252	707,620,000	30 800 000	9 240 000	52 997 920	4 620 000	0	0	805,277,920

ENEO LA UTEKELEZAJI	IDADI YA VIJJJI/ MITAA/ SHEHIA	IDADI YA KAYA	MALIPO KWA WALENGWA	MALIPO YA USIMAMIZI NGAZI YA KIJJI/ MTAA/ SHEHIA	MALIPO YA USIMAMIZI NGAZI YA MKOA	MALIPO YA USIMAMIZI NGAZI YA WILAYA NA KATA		MALIPO YA AJIRA ZA MUDA		JUMLA YA FEDHA KILA HALMASHAURI
						WILAYA	KATA	IDADI YA WALENGW A	MALIPO KWA WALENGWA	
Dodoma										
Bahi	37	7,718	408,974,000	3 700 000	1 110 000	13 928 605	555 000	10,403	455,751,849	884,019,454
Chamwino	50	17,662	532,765,000	5 000 000	1 500 000	17 804 055	750 000	25,367	1,332,054,361	1,889,873,416
Chemba	42	4,892	158,260,000	4 200 000	1 260 000	15 613 650	630 000	0	0	179,963,650
Dodoma Mjini	73	6,223	192,336,000	7 300 000	2 190 000	15 815 795	1 095 000	7,323	342,679,926	561,416,721
Kondoa	84	9,976	481,680,000	8 400 000	2 520 000	19 207 520	1 260 000	14,447	398,719,210	911,786,730
Kongwa	43	7,823	529,468,000	4 300 000	1 290 000	13 498 085	645 000	0	0	549,201,085
Mpwapwa	57	5,862	323,052,000	5 700 000	1 710 000	17 393 115	855 000	8,476	432,733,966	781,444,081
JUMLA NDOGO	386	60,156	2,626,535,000	38 600 000	11 580 000	113 260 825	5 790 000	66,015	2,961,939,312	5,757,705,137
Geita										
Bukombe	42	5,055	191,816,000	4 200 000	1 260 000	16 138 360	630 000	0	0	214,044,360
Chato	73	7,506	280,572,000	7 300 000	2 190 000	16 135 690	1 095 000	0	0	307,292,690
Geita	94	8,145	318,776,000	9 400 000	2 820 000	20 706 875	1 410 000	0	0	353,112,875
Geita Mjini	40	4,632	183,372,000	4 000 000	1 200 000	11 140 485	600 000	0	0	200,312,485
Mbogwe	65	4,140	155,520,000	6 500 000	1 950 000	14 711 800	975 000	0	0	179,656,800
Nyang'hwale	40	3,034	116,228,000	4 000 000	1 200 000	11 500 110	600 000	0	0	133,528,110
JUMLA NDOGO	354	32,512	1,246,284,000	35 400 000	10 620 000	90 333 320	5 310 000	0	0	1,387,947,320
Iringa										
Iringa	82	7,822	262,532,000	8 200 000	2 460 000	28 583 000	1 230 000	0	0	303,005,000
Iringa Manispaa	98	2,867	97,676,000	2 400 000	2 940 000	13 740 442	1 470 000	0	0	118,226,442
Kilolo	70	5,930	173,372,000	7 000 000	2 100 000	20 032 140	1 050 000	0	0	203,554,140
Mufindi	95	7,575	220,580,000	9 500 000	2 850 000	21 020 320	1 425 000	0	0	255,375,320
JUMLA NDOGO	345	24,194	754,160,000	27 100 000	10 350 000	83 375 902	5 175 000	0	0	880,160,902

ENEO LA UTEKELEZAJI	IDADI YA VIJIIJ/ MITAA/ SHEHIA	IDADI YA KAYA	MALIPO KWA WALENGWA	MALIPO YA USIMAMIZI NGAZI YA KIJIIJ/ MTAA/ SHEHIA	MALIPO YA USIMAMIZI NGAZI YA MKOA	MALIPO YA USIMAMIZI NGAZI YA WILAYA NA KATA		MALIPO YA AJIRA ZA MUDA		JUMLA YA FEDHA KILA HALMASHAURI
						WILAYA	KATA	IDADI YA WALENGW A	MALIPO KWA WALENGWA	
Kagera										
Biharamulo	50	6,905	232,412,000	5 000 000	1 500 000	16 610 100	750 000	0	0	256,272,100
Bukoba	63	8,019	260,284,000	6 300 000	1 890 000	14 060 250	945 000	0	0	283,479,250
Bukoba Manispaa	45	3,115	112,200,000	4 500 000	1 350 000	11 055 490	675 000	0	0	129,780,490
Karagwe	54	8,891	300,444,000	5 400 000	1 620 000	15 456 105	810 000	0	0	323,730,105
Kyerwa	54	7,808	285,664,000	5 400 000	1 620 000	13 703 875	810 000	0	0	307,197,875
Missenyi	50	5,745	193,928,000	5 000 000	1 500 000	13 435 125	750 000	0	0	214,613,125
Muleba	109	14,476	486,984,000	10 900 000	3 270 000	20 399 830	1 635 000	0	0	523,188,830
Ngara	52	7,702	258,172,000	5 200 000	1 560 000	13 980 500	780 000	0	0	279,692,500
JUMLA NDOGO	477	62,661	2,130,088,000	47 700 000	14 310 000	118 701 275	7 155 000	0	0	2,317,954,275
Katavi										
Mlele	28	2,581	84,444,000	2 800 000	840 000	12 291 579	420 000	0	0	100,795,579
Mpanda	24	2,018	69,884,000	2 400 000	720 000	9 171 886	360 000	2,630	126,956,526	209,492,412
Mpanda Mji	19	1,776	55,432,000	1 900 000	570 000	7 099 432	285 000	1,859	104,613,005	169,899,437
Nsimbo	13	1,000	30,576,000	1 300 000	390 000	6 191 863	195 000	1	83,946	38,736,809
JUMLA NDOGO	84	7,375	240,336,000	8 400 000	2 520 000	34 754 760	1 260 000	4,491	231,653,477	518,924,237
Kigoma										
Buhigwe	36	7,880	243,952,000	3 600 000	1 080 000	10 991 610	540 000	0	0	260,163,610
Kakonko	32	7,347	244,648,000	3 200 000	960 000	11 032 480	480 000	0	0	260,320,480
Kasulu	42	8,152	268,752,000	4 200 000	1 260 000	15 549 260	630 000	0	0	290,391,260
Kasulu Mji	22	4,783	151,272,000	2 200 000	660 000	9 044 720	330 000	0	0	163,506,720
Kibondo	40	9,573	319,076,000	4 000 000	1 200 000	19 305 000	600 000	12,094	317,885,194	662,066,194
Kigoma	32	5,064	197,120,000	3 200 000	960 000	17 055 000	480 000	0	0	218,815,000
Kigoma Manispaa	49	9,930	365,656,000	4 900 000	1 470 000	12 105 140	735 000	0	0	384,866,140
Uvinza	26	3,730	142,910,500	2 600 000	780 000	15 749 045	390 000	4,146	71,264,217	233,693,762

ENEO LA UTEKELEZAJI	IDADI YA VIJIIJ/ MITAA/ SHEHIA	IDADI YA KAYA	MALIPO KWA WALENGWA	MALIPO YA USIMAMIZI NGAZI YA KIJII/ MTAA/ SHEHIA	MALIPO YA USIMAMIZI NGAZI YA MKOA	MALIPO YA USIMAMIZI NGAZI YA WILAYA NA KATA		MALIPO YA AJIRA ZA MUDA		JUMLA YA FEDHA KILA HALMASHAURI
						WILAYA	KATA	IDADI YA WALENGW A	MALIPO KWA WALENGWA	
JUMLA NDOGO	279	56,459	1,933,386,500	27 900 000	8 370 000	110 832 255	4 185 000	16,240	389,149,411	2,473,823,166
Kilimanjaro										
Hai	43	3,836	122,200,000	4 300 000	1 290 000	11 347 870	645 000	0	0	139,782,870
Moshi	93	6,981	211,872,000	9 300 000	2 790 000	17 394 500	1 395 000	0	0	242,751,500
Moshi Manispaa	35	1,416	49,212,000	3 500 000	1 050 000	7 306 909	525 000	0	0	61,593,909
Mwanga	48	3,327	109,664,000	4 800 000	1 440 000	13 061 000	720 000	0	0	129,685,000
Rombo	43	5,112	157,900,000	4 300 000	1 290 000	11 737 635	645 000	0	0	175,872,635
Same	59	7,857	261,944,000	5 900 000	1 770 000	16 751 385	885 000	0	0	287,250,385
Siha	24	1,820	65,748,000	2 400 000	720 000	9 472 960	360 000	0	0	78,700,960
JUMLA NDOGO	345	30,349	978,540,000	34 500 000	10 350 000	87 072 259	5 175 000	0	0	1,115,637,259
Lindi										
Kilwa	59	5,205	150,140,000	5 900 000	1 770 000	22 911 750	885 000	0	0	181,606,750
Lindi	88	8,700	247,416,000	8 800 000	2 640 000	20 800 375	1 320 000	0	0	280,976,375
Lindi Manispaa	30	2,394	69,432,000	3 000 000	900 000	9 938 625	450 000	0	0	83,720,625
Liwale	46	2,785	82,568,000	4 600 000	1 380 000	12 187 840	690 000	0	0	101,425,840
Nachingwea	69	5,043	147,284,000	6 900 000	2 070 000	18 025 375	1 035 000	0	0	175,314,375
Ruangwa	52	5,886	162,548,000	5 200 000	1 560 000	14 813 460	780 000	0	0	184,901,460
JUMLA NDOGO	344	30,013	859,388,000	34 400 000	10 320 000	98 677 425	5 160 000	0	0	1,007,945,425
Manyara										
Babati	63	11,102	402,364,000	6 300 000	1 890 000	16 629 000	945 000	0	0	428,128,000
Babati Mji	21	1,037	33,972,000	2 100 000	630 000	4 891 363	315 000	0	0	41,908,363
